

---

# MALEZI

## MWONGOZO WA MKUFUNZI

Karibu katika ulimwengu wa malezi. Katika warsha hii yenyе vipindi vinne, utapata misingi ya mpango wa malezi inavyopaswa kuwa. Ijapokuwa vile vinavyofundishwa katika vipindi hivi vinne vinaweza kutumiwa katika muktadha mbalimbali ndani ya Kanisa, kusudi la mafunzo haya maalum ya malezi ni kwa wale watakaowaelekeza wapanda Kanisa walio kwenye mafunzo.

## YALIYOMO

<b>Kipindi cha 1</b> MALEZI NI NINI?.....	3
<b>Kipindi cha 2</b> KUMLEA MTU MZIMA.....	12
<b>Kipindi cha 3</b> UHUSIANO WA MALEZI.....	22
<b>Kipindi cha 4</b> MAMBO YA MSINGI KUHUSIANA NA MALEZI.....	34
<b>KITABU CHA</b> MLEZI.....	40
<b>ABC ZA MPANDA</b> KANISA.....	42

**Multiplication Network Ministries| 2013**

Toleo la Mwisho 03/04/2013  
Isipokuwa imeelezwa bayana, Maandiko yote  
yametolewa katika tafsiri ya New International  
Version

MWONGOZO WA MKUFUNZI | MALEZI

## **KIPINDI CHA KWANZA MALEZI NI NINI?**

Kulingana na Sura ya 1 ya Kitabu cha *Why We Must Mentor Church Planters*  
na Sura ya 1 ya *Masterful Mentoring*



### **UTANGULIZI**

Katika semina hii utajifunza mchakato wa kuwalea wapanda Kanisa kwa mafanikio. Kusudi ni kutoa nyenzo zinazohitajika kuhakikisha gharama za utumishi, raslimali, na muda vinapelekea kuzaliwa kwa Kanisa jipya linalomletea Mungu utukufu. Upandaji wa Kanisa wenye mafanikio, wenye afya mara nyingi hupanua ufalme wa Mungu.

Kipindi cha kwanza kinatoa dhana tatu muhimu zinazotoa msingi wa kuelewa mchakato wa malezi. Washiriki watapitia dhana tatu za msingi zinazohusiana na malezi, kutambua misingi ya kitheolojia ya malezi, na kupitia mifano ya kibiblia iliyochaguliwa kwa habari ya malezi.

### **KUELEZEA "MALEZI"**

Elezea kwamba matumizi ya maneno mlezi na malezi/kulea katika biashara na elimu yanatupatia uelewa wa kawaida wa maneno haya. Waweza kujiuliza, kwa nini basi ni muhimu kuielezea dhana hii hapa? Pendekeza majibu yafuatayo:

1. Tafsiri sahihi inafafanua dhana na kutoa picha halisi ya kiufahamu ya mchakato, watu wanaohusika, na majukumu yao.
2. Kwa kubainisha lengo mahsus, dhana zisizo sahihi hubadishwa kwa dhana sahihi \*
3. Tafsiri ifaayo hutoa namna sahihi ya kupima utendaji wa washiriki kwa awamu zote za mchakato wa malezi.

Tafsiri zifuatazo za malezi zinatutoa kutoka tafsiri rahisi kwenda tafsiri ngumu. Ipitie kila moja na ufikirie matumizi ya kila dhana iliyoelezwa. Waalike washiriki kupigia mistari vidokezo muhimu vya malezi walivyopata katika tafsiri na ndipo waombe washirikishe kile walichobaini.

### **TAFSIRI RAHISI**

Tunaanza na tafsiri hii rahisi: Malezi ni UHUSIANO wa kudumu, wa MAKUSUDI ambao kwa huo mtu mmoja huwekeza UZOEFU, UJUZI, na UFAHAMU ili kukuza uwezo na ujuzi wa mtu mwagine.

Waandishi Paul Stanley na J.Robert Clinton wanaelezea malezi kuwa " ni uzoefu wa kimahusiano ambao kwa huo mtu mmoja HUMWEZESHA mtu mwagine kwa kumshirikisha RASLIMALI zilizotolewa na Mungu" (1992:33). Wanapanua tafsiri kwa kuongeza vidokezo kadhaa vilivyo ndani ya uhusiano wa malezi.

Malezi ni mchakato wa kimahusiano ambao kwa huo mlezi, anayejua au mwenye uzoefu wa kitu fulani, anakihamisha hicho kitu(raslimali ya hekima, habari, ujasiri, utambuzi, mahusiano, hali,nk) kwa mlelewa,kwa wakati na kwa njia mwafaka, ili kwamba kiweze kurahisisha maendeleo au uwezesho(1992:40).

MWONGOZO WA MKUFUNZI | MALEZI

Shughuli:

- A. Waombe washiriki kushirikisha kile walichopigia mstari. Andika mawazo ya msingi au vifungu juu ya ubao au kipande kikubwa cha karatasi.
- B. Waulize mmoja wa washiriki aeleze maana au kushirikisha mfano wa vifungu vyaa msingi walivyobainisha. Hakikisha wanataja yafuatayo:

DHANA MUHIMU:

- 1. Malezi ni mchakato wa kimahusiano 2. Mlezi ana uzoefu wa kushirikisha
- 3. Kitu fulani kinahamishwa 4. Mlezi huchochea maendeleo 5. Mlezi huwezesha

Kisha, waombe washiriki kusoma tafsiri ya pili na kuangalia inavyofanana na ile tafsiri ya awali na maoni mapya. Tafsiri inatoka kwa Jim Osterhouse na Gary Teja kwenye kitabu chao cha *Masterful Mentoring*.

Kwa nia na makusudi yote....malezi [ni] shughuli ya kumsaidia mtu mwengine ili akue katika ujuzi,tabia,na maarifa katika eneo lolote la maisha.Mara nyingi inaonyesha mtu mmoja kati ya wawili anakuwa na uzoefu zaidi, mwenye maarifa zaidi, na kwa hiyo ana kitu fulani cha kuhamisha kwenda kwa mdogo,mwenye uzoefu mdogo, mwenye maarifa kidogo. Mfumo wa utoaji kwa namna ya " uhamishaji" ndio tunaouita malezi(2012:3)

Shughuli: Waombe washiriki ambao wamepitia uhusiano wa malezi rasmi waeleze jinsi uzoefu wao unavyolanganishwa na tafsiri ya waandishi. Vikundi vilinganishe tafsiri. Unaweza kutumia maswali haya kuelekeza na kulenga mjadala:

Ni kwa namna gani tafsiri zinafanana?  
Ni mawazo gani yaliyo pande zote?  
Tafsiri ya pili inatoa mawazo gani mapya kwa habari ya malezi?

Unaweza kuuliza maswali ya nyongeza ili kuweka bayana vidokezo lengwa vyaa tafsiri hizi:

Nini maana ya "mchakato wa kimahusiano"?  
Ni nini lengo la mchakato wa malezi, kulingana na waandishi hawa?  
Ni maeneo gani ya maisha na uzoefu yanahusishwa katika malezi?  
Je, maelezo ya "huchochea maendeleo au kuimarishe" yanatuambia nini kwa habari ya mchakato wa malezi?

#### KUMWELEZEA "MLEZI"

Neno Mlezi lilianzia kwenye shairi bora la Homer, liitwalo Odyssey. Odysseus alipoondoka kwa ajili ya vita ya Trojan, alimkabidhi mwanawee, Telemacus, chini ya uangalizi wa mtumishi mwenye hekima na wa kuaminika,

Mlezi. Mlezi aliwajibika kuongoza maendeleo ya kijana kijamii, kielimu, na maandalizi ya maisha. Kwa hiyo, mlezi kwa kawaida anatafsiriwa kama mshauri mwenye hekima na wa kuaminiwa na mwalimu.

Hii inaelezewa katika ufanuzi wa kamusi: "ni mshauri wa kuaminiwa au mwongozaji." Inaeleza kwamba *mwelekezaji* na *kocha* ni maneno yenye maana zinazofanana.<sup>1</sup> Kwa makusudi yetu, mlezi ni mtu mwenye uzoefu anayeingia katika uhusiano wa kimaendeleo na mtu mwenye uzoefu mdogo kwa kusudi la kukuza uwezo, ujuzi, mitazamo ya mtu huyo na makuzi ya kiroho kuhusiana na huduma.

Shughuli: Kama sehemu ya ufanuzi wao, Osterhouse na Teja wanatumia maelezo au maneno ya picha, kuelezea mlezi. Fafanua jinsi ambavyo kila moja inachangia tafsiri ya mlezi.

- Mkunga
- Mwanafunzi mwenza
- Mwonyesha njia
- Mtoa ramani ya maisha
- Kocha
- Mlinzi
- Mkuzaji wa watu

#### KUELEZEA "MLELEWA"

Waelezee washiriki kwamba kabla ya mwaka 1978 maneno *mwanafunzi* yalitumika kuelezea mtu wa pili katika uhusiano wa malezi.<sup>2</sup> Kila moja ya maneno haya inatoa maana za utegemezi na kutawaliwa au kulindwa na mlezi ambayo haichangii kuleta ufahamu wa dhana yake kuhusiana na huduma ya upandaji wa makanisa. Ndiyo tumeamua kutumia "mlelewa" kama neno linalofaa kuelezea mtu wa pili katika uhusiano wa malezi. Pitia tafsiri ifuatayo ya mlelewa kutoka kitabu cha *Masterful Mentoring*, kisha tumia vifungu vyatubu chini kuwasadia washiriki kuelewa asili ya mlelewa.

*Mlelewa pia ni mwanafunzi aliyekua/mtu mzima. Kama mtu mzima, anayo majukumu fulani ya kufanya yaliyo tofauti na ya mlindwa (anayelindwa) au mtoto anayehitaji kulishwa kwa kijiko. "Kiini cha uhusiano bora sasa kinaongozwa na mlelewa zaidi kuliko mlezi." Kwa maneno mengine, neno mlelewa linalezea njia tofauti ya namna ya kuuchukulia mchakato wa malezi na uhusiano wa malezi. Mlelewa sio mtu mtendewa katika mchakato huu, bali mtendaji zaidi. Mlelewa ni "mtu anayefanya jitihada kupanga, kumiliki, na kutumia ipasavyo maarifa, ujuzi, utambuzi, mitizamo au hekima iliyotolewa ... anayeibua nje msaada huo na kuutumia inavyotakiwa kwa makusudi ya maendeleo popote unapohitajika." Mlelewa*

---

<sup>1</sup> Merriam Webster's Tenth Collegiate Dictionary.

<sup>2</sup> Osterhouse and Teja 2012:8

*sio kiumbe cha mtu fulani tu; bali ni mtu anayesaidiwa njiani ili kuukuza upekee wake.<sup>3</sup>*

- 1.Mlelewa ni mwanafunzi **MTENDAJI** anayejua hitaji la utambuzi wa **NYONGEZA** na ushauri katika kukuza ujuzi wa kihuduma na maarifa.
- 2.Mlelewa ni "mtu mzima ambaye kwa **UFAHAMU** amepitia safari ya kimaendeleo."<sup>2</sup>
- 3.Mlelewa ni **MTENDAJI** zaidi kuliko mtendewa katika mchakato huu.
- 4.Mlelewa hufanya jitihada ili **KUTAFITI, KUMILIKI,** na **KUTUMIA** ipasavyo maarifa , ujuzi, utambuzi,mitizamo, au hekima iliyotolewa.
- 5.Mlelewa **HUTAFUTA MSAADA** na kuutumia ipasavyo kwa makusudi ya maendeleo popote unapohitajika.
- 6.Mlelewa ni mtu anayesaidiwa njiani ili kukuza **UPEKEE** wake.
- 7.Uhusiano wa malezi yaliyo bora unaongozwa na **MLELEWA** zaidi kuliko mlezi.

Shughuli: Wagawe washiriki katika vikundi vidogo. Wape kazi ya kusoma ufanuzi wa Osterhouse na Teja juu ya mlelewa uliotolewa juu na waujadili namna unavyochonga uelewa wetu wa malezi kwa kufanya yafuatayo:

- A. Tumia maneno yako kuelezea tena tabia za mlelewa zilizoorodheshwa juu. Je, kuna tabia nyininge ungependa zielezewe?
- B. Ikiwa uhuisiano unaongozwa na mlelewa, ni nini jukumu la mlezi?

#### MWANAFUNZI, MLEZI, KOCHA

Katika hatua hii, yaweza kuwa muhimu kubainisha baadhi ya dhana ambazo zinaweza kuwachanganya kwenye mijadala muhimu ya malezi. Katika agizo la mwisho la Yesu, aliwaelekeza wafuasi wake kuwafanya mataifa yote kuwa wanafunzi. Je,kufanya wanafunzi na kulea kuna maana sawa na kunafikia malengo yale yale? Baadhi ya waandishi wanaona uanafunzi kama mchakato endelevu (wa maisha yote) wa kukua kiroho, wakati wengine wanauona kama mafunzo ya awali katika maisha ya Kikristo. Wengine wameelezea malezi kama uanafunzi endelevu (Brown 2012:48). Ni katika hatua ipi uanafunzi hufungua njia ya malezi?

Tuna FUNDISHA WAUMINI WAPYA-MSINGI: kuweka misingi  
Tuna LEA VIONGOZI WANAOIBUKIA-MUUNDO:kutoa muundo wa uongozi.

Tuna KOCHI WATENDAJI WA HUDUMA-UWEZESHAJI:kuwasaidia wazae matunda. Shughuli: Pitia tofauti kati ya maneno haya kwenye kitabu cha Masterful Mentoring ikiwa umekizalisha\*\*kitabu. Wanafunzi wajadili maneno na kubainisha kati ya aina za huduma muhimu kwa kila hatua ya maendeleo ya uongozi. Washiriki watoe mifano ya kitu gani watu wanaweza kujifunza katika aina tatu za mafunzo yaliyorodheshwa hapo juu.

<sup>3</sup> Osterhouse na Teja 2012:8.

<sup>4</sup> Laurent Daloz 1986:206.

## MISINGI YA KITHEOLOJIA KWA AJILI YA MALEZI

Kipengele hiki kimegawanyika sehemu tatu. Katika sehemu ya kwanza utapima jinsi Mungu kama Utatu anavyotoa misingi ya uhusiano kwa wanadamu. Sehemu ya pili inaelezea ushirika wa kanuni hii katika uumbaji wa Mungu kwa wanadamu. Sehemu ya tatu inachunguza kufanyika mwili kwa Yesu na huduma kama kielelezo chetu kwa matumizi ya tabia hizi katika kuwalea wengine.

## MISINGI KATIKA ASILI YA UTATU

Katika kipengele hiki utawasaidia washiriki kuelewa jinsi asili ya Utatu inavyohusiana na jukumu letu la kuwalea wapanda Kanisa wapya. Kwanza, elezea kwamba huu ni mfano halisi wa namna ambayo Mungu amejifunua mwenyewe kwetu. Ijapokuwa neno Utatu halipatikani katika Biblia, dhana ya asili ya utatu ya Mungu imetolewa katika vifungu vingi bainifu vya Biblia. Kanisa liliasili neno hili kuelezea jinsi Mungu alivyojifunua kama Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Pili, elezea kwamba uhusiano ndani ya Utatu unahusisha watatu walio katika umoja mkamilifu na wote wakiwa sawa, wote wa milele, na wasiotenganishwa. Tumia ufanuzi huu wa Utatu kwa malezi kwa namna ifuatayo:

- . Kwanza, Mungu ni **PENDO**. Hali ya msingi ya asili ya Mungu ni upendo wake wa kujitolea mwenyewe.
- . Pili, Utatu unakaa katika **JAMII** ya milele inayopambanuliwa kwa upendo na umoja.
- . Tatu, Mungu ana uwezo wa **UHUSIANO** ndani ya Utatu na pia pamoja na viumbe wake.
- . Nne, Mungu **ANAWAJALI** watu na viumbe vyote

Sifa hizi za asili ya Mungu zinaakisiwa ndani ya wanadamu aliowaumba.

Shughuli: Waombe washiriki kutoa mifano ya namna walivyoona asili ya Mungu ikiakisiwa kwenye uumbaji wake. Ni jinsi gani sifa hizi za asili ya Mungu zinavyohusiana na malezi yetu?

## MISINGI KATIKA UUMBAJI WA MUNGU

Asili na tabia ya Mungu inaakisiwa katika shughuli yake ya uumbaji. Upendo wake na uwezo wake katika uhusiano ulimsukuma kuumba ulimwengu kuwa chombo chake cha upendo na uangalizi. Aliumba kila kitu kilichopo pasipo kitu kwa utukufu wake na kama alivyopenda mwenyewe. Uumbaji unadhihirisha ukarimu wa Mungu unaotolewa kwetu\*\*\*. Yeye hutenda kwa manufaa ya wengine. Kama msisitizo wa sifa hii, aliwaumba wanadamu kwa sura na mfano wake; mwenye uwezo wa kupenda, kuishi katika jamii, na kuwa na uhusiano na wengine.

Hivyo, Mungu aliwaumba wanadamu kwa ajili ya jamii na uhusiano. "Utatu" wa Mungu na vyote vinavyohusiana nao vinatoa kielelezo kwa mahusiano ya wanadamu. Mungu hakuumba tu- ana uhusiano na uumbaji wake.

Wanadamu, wameumbwa na Mungu wakiwa na uwezo wa kipekee:

1. Wameumbwa ili **KUPENDA**:

- Kumpenda Mungu
- Kuwapenda jirani zao

2. Wanadamu wameumbwa kwa ajili ya **JAMII**:

- Kuishi kwa upendo na usawa na wanadamu wengine, wakidhihirisha mfano wa umoja wa Utatu
- Jamii ni udhihirisho mkamilifu wa uhusiano wenye upendo

3. Wanadamu wameumbwa kwa ajili ya **UHUSIANO**:

- Na Muumbaji wao
- Na ulimwengu ulioumbwa. Uhusiano huu uliotolewa na Mungu unahusisha wajibu wa kutawala na kuujali ulimwengu ulioumbwa.
- Na wanadamu wengine

4. Wanadamu wameumbwa na uwezo na wajibu wa **KUWAJALI** watu wengine na vitu vilivyoumbwa, sio wao wenyewe tu.

- Mkazo wa uumbaji wa Mungu uko wazi, ukiwaelekea wengine.

Swali la Mjadala: Ni kwa namna gani kuumbwa kwa sura na mfano wa Mungu kunaathiri vile tunavyohusiana na watu wengine?

Kadiri tunavyozidi kugezwa kwa sura ya Mungu katika Kristo Yesu, ndivyo tunavyozidi kuakisi pendo lake na uwezo wake wa kuishi na jamii. Je, itakuwaje pale sura ya Mungu itakapodhihirishwa ndani ya mtu katika huduma yake? (Baadhi ya mifano: uvumilivu kwa mtu mgumu/jeuri, msamaha kwa mshirika ambaye amemkwaza ndugu katika Kristo, kuambiana ukweli katika upendo.)

Shughuli: Chagua washiriki tofauti ili wasome vifungu hivi vitano va Biblia: Yohana 3:16; Mathayo 20:28; Marko 10:45; Yohana 10:11, na Wafilipi 2:5-11. Baada ya kila kifungu kusomwa, waombe washiriki wengine waelezee kila kimoja kinatuambia nini juu ya kufanyika mwili. Je, Yesu alivitumiaje katika mafundisho yake juu ya ukuu katika ufalme wa Mungu? Je, haya yanaweza kutumiwaje katika malezi?

Mungu alikuja **KUKAA** pamoja na **WATU** katika umbo linaloonekana kupitia kufanyika mwili. Yesu, aliyezaliwa na Bikira Maria, ni Emanueli, Mungu pamoja **NASI**. Alitumwa ulimwenguni kupitia upendo wa Mungu. Alikuja kumfunua **BABA** kwetu. Ingawa ni Mungu aliyefanyika mwili, alituambia kwamba alikuja kutoa, sio kutumikiwa; alikuja kuyatoa maisha yake kwa ajili ya wengine (Mathayo 20:28; Marko 10:45; Yohana 10:11; Wafilipi 2: 2:5-10).

Kwa kuja kwetu katika umbo la kibinadamu, Yesu alidhihirisha namna ambavyo Mungu alikusudia kutumia uwezo wetu aliotupatia kama wanadamu - ku **PENDA**, ku**HUSIANA**, kujenga **JAMII**, na kuwatumikia **WENGINE** kwa faida ya ufalme wa Mungu. Alitimiliza hili kwa kuingia katika

uhusiano na kujenga jamii pamoja na wanafunzi wake. Marko anatuambia kwamba kutoka kati ya wafuasi wake walio wengi, Yesu alichagua wanaume kumi na wawili, "akawaita mitume" kwa makusudi mawili. Kwanza, "wapate kuwa pamoja naye," na " kwamba awatume kuhubiri , tena wawe na amri ya kutoa mapepo" (Marko 3:14-15). Hapa kipaumble kinatolewa kuwa katika **UHUSIANO** pamoja naye<sup>5</sup>. Hali akijua muda mfupi aliokuwa nao wa kuwashudumia ,Mchungaji Mwema alitumia muda wake mwingu akiwalea kumi na wawili, akiwafundisha, akiwafanulia, na kuwawezesha kuiendeleza kazi yake baada ya Yeye kuondoka. Kwa maneno yake ya mwisho, aliwaagiza **KUWALEA** wengine kama yeye alivyowalea (Mathayo 28:19-20; Yohana 20:21).

## MIFANO YA KIBIBLIA YA MCHAKATO WA MALEZI

Simulizi nyingi katika Maandiko zinadhahirisha mchakato wa kulea,wakati mipango ya Mungu ikitimilizwa na wanadamu wanaoongozwa na kuwezeshw na Roho Mtakatifu. Kizazi kimoja hutumikia kizazi kingine. Wazazi huwafundisha watoto wao kumjua Mungu ili kuumba kizazi cha wacha Mungu. Kiongozi huwaelimisha warithi wake katika njia za Mungu na uongozi. Simulizi ni nyingi mno kiasi cha kutoweza kutosha hapa, hivyo tutalenga mahusiano ya aina tatu kati ya mlezi na mlelewa ambayo yanatumika kufafanua msingi wa malezi.

Kwa pamoja na washiriki, rejeeni vidokezo vitano vya Clinton na Stanley vinavyoeleza maana ya malezi: (1)malezi ni mchakato wa kimahusiano; (2) mlezi ana uzoefu wa kushirikisha ; (3) kitu fulani kinahamishwa; (4) mlezi huchochea maendeleo; (5) mlezi huwezesha. Tumia vidokezo hivi kama muundo wa kupima mchakato wa malezi kwa kila mifano ya kibiblia inayofuata. Maeleo makamilifu zaidi kwa kila mfano yametolewa katika Somo la *Kwa nini tuwalee wapanda Kanisa* yanayopatikana katika Kifaa cha Nyenzo za Malezi.\*\*

## MUSA NA YOSHUA

Kwanza utapima kisa cha Musa na Yoshua mrithi wake<sup>6</sup>, katika uhusiano uliodumu kwa miongo minne. Unaposoma vifungu vifuatavyo, angalia vidokezo muhimu anavyotumia mwandishi kuelezea simulizi yake. Kwa kuwa wahusika wote ni wa muhimu katika simulizi ya Kutoka na makazi ya Nchi ya Ahadi,shughuli ifuatayo ya vikundi itawasaidia washiriki kukamata vidokezo vitano vya simulizi.

Shughuli: Washiriki mmoja mmoja au katiika vikundi vidogo, wasome vifungu vilivyochanguliwa kutiika kwenye vifungu muhimu kwa habari ya uhusiano kati ya Musa na Yoshua. Inaweza kufaa zaidi ukiwapa kazi ya kusoma kwa kikundi. [ Kutoka 17:9-14; 24:13-18; 32:17-18; 33:11; Hesabu 11:24-29; 14:6-9, 30,38; 27:18-23; 32:12; 34:17; Kumbukumbu 1:38; 3:21-22, 28; 31:3,7-8, 14, 23; 32:44-46; 34:9; Yoshua 1:1-18; 24:31; Waamuzi 2:7-11]. Baada ya kusoma,wana vikundi wajibu maswali yafuatayo:

<sup>5</sup> Dhana hii imejengwa katika *The Training of the Twelve* na A.B.Bruce(1971) na

The Master Plan of Evangelism na Robert E.Coleman (1963).

<sup>6</sup> Angalia mfano ulivyoolezwa katika *Kwa nini Tuwalee wapanda Kanisa*(uk.17-18).

1. Eleza jinsi uhusiano wa Musa na Yoshua ulivyokua.
2. Ni ujuzi gani ama uzoefu aliokuwa nao Musa ambao Yoshua aliuhitaji?
3. Ni jinsi gani Musa alihamisha ujuzi na uzoefu wake kwa Yoshua?
4. Ni kwa namna gani Yoshua aliendelea au alikuwa kama matokeo ya uhusiano wake na Musa?
5. Je, Musa alimwezeshaje Yoshua?
6. Je, matokeo ya mwisho ya watu wa Mungu yalikuwa ni yapi?

#### BARNABA NA SAULLI WA TARSO

Barnaba na Sauli wanabeba mwanga wa simulizi ya pili ya malezi unayokwenda kuitafakari. Miaka mitatu baada ya badiliko lake huko Dameski, Sauli wa Tarso alisafiri Yerusalem ili kukutana na mitume (Gal.1:18). Hata hivyo, waumini wa huko hawakuwa na imani kuwa mtesaji wao wa awali alikuwa sasa ni muumini mwenzao katika Kristo. Hapa, Barnaba alianzisha uhusiano wa malezi na Sauli. Barnaba alihatarisha ushuhuda wake ili kufanyika kiunganishi ambaye kwa yeye, Sauli, muumini akapokelewa katika ushirika wa mitume na waaminio.

Baadaye, mitume walimtuma Barnaba kuliangalia, kulitia moyo, na kuliimarisha kusanyiko jipya la waumini Wamataifa huko Antioquia. Mara akaona fursa ya kuikuza zaidi huduma ya Sauli, na akamleta Sauli kutoka Tarso kuja Antioquia. Huko, akiwa na Barnaba kama mlezi wake, Sauli akaanza kuchanua katika huduma yake. Barnaba alikuwa bado akimlea Sauli pale Roho Mtakatifu alipowachagua kwa ajili ya huduma ya kimishonari. Barnaba anadhihirisha hatua muhimu katika mchakato wa malezi kwa kumruhusu Sauli (sasa akiitwa Paulo) apokee jukumu jipya la uongozi. Kwa uongozi wa Roho Mtakatifu, alimwachia mlelewa wake jukumu ambalo kwalo Paulo aliitiwa. Kujuu muda mwafaka wa kumwachilia mwanafunzi ni hatua muhimu sana kwa malezi yenye mafanikio.

Kazia funguo za msingi za malezi zilizopo kwenye simulizi hii.

- Barnaba ni jina lililotolewa na mitume likimaanisha "mwana wa faraja" ( Mdo 4:36)
- Uhusiano wa malezi ulianzishwa na Barnaba (Mdo 9:27)
- Aliona ama alielewa uwezo wa Sauli kwa ajili ya Ufalte wa Mungu (Mdo 9:27-29)
- Alipata mahali pa huduma kwa ajili Sauli na kushiriki huduma pamoja naye (Mdo 11: 25-26 )
- Aliweka mfano ambao baadaye Paulo aliweza kuuzalisha katika huduma yake mwenyewe ( 1 Korintho 11:1; 2Timotheo 2:2).
- Aliweza kumruhusu Paulo kuchukua nafasi ya uongozi (Mdo 13:7-46).
- Barnaba pia alimlea Yohana Marko, ambaye sambamba na Paulo waliandika theluthi ya Agano Jipya.

Shughuli: Mwombe mshiriki mmoja au wawili watumie maswali yaliyopo chini kuelezea jinsi Barnaba aligomlea Paulo.

1. Eleza jinsi uhusiano kati ya Barnaba na Sauli/Paulo ulivyokua.
2. Ni ujuzi gani ama uzoefu aliokuwa nao Barnaba ambao Paulo aliuhitaji?

3. Ni jinsi gani ujuzi au uzoefu huo ulihamishwa kwa Paulo?
4. Ni kwa namna gani Paulo aliendelea ama alikua kama matokeo ya uhusiano wake na Barnaba?
5. Je, Barnaba alimwezeshaje Paulo?

## UTENDAJI WA MALEZI WA PAULO

Paulo alizalisha malezi aliyyapokea kutoka kwa Barnaba katika safari zake zote za umisheni zilizofuata. Katika kitabu cha Matendo na katika Nyaraka za Paulo, watu kumi na sita wametajwa kama watu waliowahi kufanya kazi na Paulo. Luka anawataja saba wengine kama watenda kazi wenzake katika safari moja au zaidi za kimisheni. Hakuna shaka kabisa kwamba wote hawa walinufaika na maelekezo yake na uhusiano wake pamoja nao. Upendo wa dhati anaouonyesha kwao katika nyaraka zake unathibitisha hilo. Wazee walioliongoza Kanisa huko Efeso walikuwa ni matokeo ya malezi ya Paulo, kwani ndio waliokuwa viongozi wa makanisa saba ya Asia. (Mdo 19:10; Ufu 2-3). Kwa watu wawili hasa, Timotheo na Tito, Paulo baadaye aliandika nyaraka zake akitoa muhtasari wa maudhui ya maelekezo yake binafsi. Paulo anawaelezea wote kama "wanangu katika imani", inawezekana akionyesha kwamba walikuwa waongofu wake. Chunguza kitabu cha Matendo, Nyaraka za Paulo, na Nyaraka kwa Timotheo na Tito ili kugundua asili ya malezi kuhusiana na walelewa wake wanaofahamika zaidi: Matendo 16:1-5; 17:14; 19:22; 20:4; 1 Wakorintho 1:1, 19; 7:5-16; 8:6, 16-24; 12:18; Wagalatia 2:1-3; Wafilipi 2:19-22; 2Wathesalonike 3:1-3,6; 1Timotheo 1:2,18-20; 2Timotheo 4:10; Tito 1:4-5.

Shughuli:

1. Elezea mahusiano aliyotumia Paulo kuwakuza viongozi vijana.
2. Paulo alifahamu na alipitia uzoefu wa vitu gani ambavyo Timotheo na Tito walihitaji kuvifahamu?
3. Ni kwa jinsi gani ujuzi na uzoefu huo ulihamishwa kwa Timotheo na Tito?
4. Ni kwa namna gani Timotheo na Tito walikua kama matokeo ya uhusiano wao na Paulo?
5. Je, Paulo aliwawezeshaje walelewa wake?

## MUHTASARI NA MAREJEO

Katika kufunga, tulipitia tafsiri zinazohusiana na malezi; Pia tulielewa misingi yake ya kithiolojia na tukapitia vifungu vilivyochanguliwa kwa habari ya malezi.

Shughuli: Waalike washiriki wapitie maudhui yote ya kipindi kwa kufanya yafuatayo.

- Washiriki waorodheshe vidokezo muhimu vya malezi kutoka katika kipindi hiki
- Waombe washiriki watoe Muhtasari wa misingi ya kitheolojia ya malezi
- Waombe washiriki kutoa neno au kifungu cha maneno kinachojumuisha masomo yaliyofundishwa kutoka kwenye mifano ya kibiblia ya malezi.
- Washiriki wabaini kidokezo cha malezi wanachovutiwa nacho zaidi na kidokezo cha malezi ambacho wanaona kinaleta changamoto zaidi.

## KIPINDI CHA PILI

### KUMLEA MTU MZIMA

Imetokana na *Kwa nini Ni Muhimu Kumlea Mpanda Kanisa?*

### UTANGULIZI

Katika somo hili utashughulika na mpanda kanisa kama mtu mzima. Utapitia mitindo ya kujifunza , dhana za kimsingi kwa mwanafunzi aliye mtu mzima, kanuni saba na faida za kufanya kazi na mtu mzima, changamoto zinazomkabili mlelewa, na manufaa ya mchakato wa malezi.

Walelewa wetu ni wapanda Kanisa. Kwa kuwa ni watu wazima, si watu wasio na chochote vichwani mwao wanaohitaji kujazwa na maarifa. Kila mmoja amepitia maisha yenye uzoefu unaofaa katika kufanya maamuzi sahihi na kama nyenzo kwa ajili ya kuandaa na kutathimini taarifa au ujuzi mpya.Wengi wao, hata hivyo,wanakosa ujuzi katika upundaji wa Kanisa na huduma ya Kichungaji. Wote wana mahitaji binafsi, njia pekee za kujifunza, na ina aina fulani ya maarifa. Sababu zote hizi ni muhimu kuzifikiria kadiri walezi wanavyotembea na wapanda Kanisa bega kwa bega katika mchakato wa upandaji wa Kanisa.

Walelewa wamechagua kuingia katika awamu mpya ya mafunzo ya huduma.Ulimwengu wa upandaji kanisa haufahamiki kwa sehemu kubwa. Wanahitaji kukuza ujuzi mpya na kupanua maarifa yao ya msingi. Watafute ushauri wa hekima ili kuwezesha ukuaji wao. Wale wanaotumika kama walezi wao wanahitaji kuingia katika uhusiano huu wakiwa na ufahamu wa namna bora ya watu wazima kujifunza.

Kumbuka kwamba walezi unaowafunza vilevile ni watu wazima. Kila kitu kilichojadiliwa hapa chini kwa habari ya walelewa kinawahu su na walezi pia.

**Shughuli:** Waombe washiriki kubaini tofauti kuu kati ya kuwafundisha watu wazima na kuwafundisha watoto. ( Utarejea orodha ya tofauti hizi baadaye katika kipindi.)

### MITINDO YA KUJIFUNZA<sup>7</sup>

Wapanda Kanisa walelewa wanawakilisha kundi la watu mbalimbali, kila moja likiwa na uwezo na mahitaji tofauti. Tunatumia neno *mitindo ya kujifunza* ili kuelezea namna ambayo kila mtu anachakata taarifa mpya. Unapaswa kuhakikisha kwamba washiriki wanatambua kwamba kila mtu hajifunzi kwa njia moja: mitindo ya kujifunza ni ya asili kwa kila mmoja, na uzoefu wa kujifunza hukuzwa kwa ujuzi wa kupokea taarifa mpya kwa mwanafunzi binafsi, akitumia mbinu mbalimbali ili kuwezesha ufahamu na utunzaji wa yale anayojifunza. Mitindo iliyotajwa chini inawakilisha ile ambayo kwa kawaada inatambuliwa mara nyingi sana na watafiti. Maeleo haya yanawasaidia walelewa kubaini mitindo yao ya kujifunza ili kukuza thamani ya uhusiano wa malezi.

---

1. Masomo katika kipengele hiki yamechukuliwa kutoka kwa Rochester Institute of Technology, " Adult Learners' Characteristics"( 2012) na Sharon G.Fisher, *Adult Learning Principles Workshop* (1989).

**Mtindo wa kujifunza kwa KUSIKILIZA:** Wanafunzi hawa hufanya vizuri zaidi pale taarifa inapotolewa kwao kwa mfumo wa maneno. Wanapata kiwango kikubwa sana cha kukumbuka na kutunza kwa njia ya hotuba na majadiliano. Wanaweza kusoma kwa sauti au kutumia kinasa sauti ili wasikilize tena ujumbe kama njia ya kuwezesha kujifunza.<sup>8</sup>

**Mtindo wa kujifunza kwa KUONA:** Wanafunzi hawa hujifunza vizuri mno pale taarifa zinapofafanuliwa au kuelezwa kwa mtindo wa kuona. Wana uwezo wa juu sana wa kukumbuka kutokana na michoro, picha na mafafanuzi. Mara nyingi hupenda kukaa katika safu za mbele ili waone kila kitu. Wanafasiri lugha ya mwili wa mzungumzaji kama sehemu ya uzoefu wao wa kujifunza.

**Mtindo wa kujifunza kwa KUGUSA:** Wanafunzi hawa vilevile wanaitwa wanafunzi wa mguso. Ni wanafunzi wanaohusika na ugunduzi ambaeo uwezo wao huongezeka kuitia mguso and majaribio lakin hukutana na ugumu sana wanapojojifunza kwa kusoma au kusikiliza. Wanastawi zaidi "mikono" inapotekeleza mbinu za maelekezo kama vile majaribio ya kemia au igizo. Mara kwa mara watachora chora au kufanya shughuli nyingine kama hizo ili kuongeza ufahamu wao wakati wanawasiliza wahadhiri.

**Mtindo wa kujifunza kwa MAZINGIRA:** Wanafunzi wa kimazingira wanahitaji kuyatawala mazingira yao. Hali ya utulivu ya mandhari, mwanga, na kiwango kizuri cha hali joto huongeza uwezo wao kutengeneza na kutunza taarifa mpya.

#### **Shughuli:**

1. Mwalike kila mtu abaini mtindo wake wa kujifunza na afikiri jambo fulani kutokana na uzoefu wake binafsi linalounga mkono. Mruhusu mshiriki mmoja au wawili waelezee jinsi ujuzi huu unavyowasaidia wao na wengine kujifunza.
2. Waulize washiriki namna wanavyoweza kuwasaidia walelewa wao kupambanua mitindo yao ya kujifunza.
3. Waulize washiriki namna wanavyoweza kuibadili mitindo yao ya malezi ili iendane na mitindo ya kujifunza ya walelewa wao.

#### **TABIA YA WANAFUNZI WALIOKUA/WATU WAZIMA**

Waeleze washiriki kwamba katika kipindi hiki mtapitia malezi yanavyohusiana na tabia, mahitaji, na uwezo wa watu wazima wanaojifunza. Hii inaibua swali jingine: Ni kwa namna gani malezi yanatofautiana na mafunzo na makuzi ya watu wazima kwa kutumia mbinu za elimu ya asili au ya kimapokeo?

Sisitiza kwamba uchunguzi mfupi wa namna watu wanavyojifunza unatoa majibu ya nguvu sana.

1. UFUNDISHAJI ni sanaa, sayansi, au taaluma ya kufundisha. Ni neno lenye maana zaidi ya moja linalotokana na maneno ya Kiyunani paidos, au "mtoto," na ago, likimaanisha "kuongoza," kwa tafsiri ya kawaida kuongoza ama kumfundisha mtoto. Kwa kawaida linatumika kurejea mbinu na mikakati ya maelekezo. Hata hivyo, utafiti wa hivi karibuni wa elimu ya watu wazima,

---

<sup>8</sup>

Thelushi mbili ya ulimwengu ni wanafunzi wa kusikiliza.

umeonesha kwamba namna za kujifunza kwa mtu mzima ni tofauti kabisa na zile za watoto na vijana. Ugunduzi huu umepelekea kutambulishwa kwa mbinu mpya ya elimu ya watu wazima iitwayo *uchangiaji*.

2. **UCHANGIAJI** ni nidhamu ya kitaaluma inayoshughulika na nadharia na mafunzo ya kiutendaji na makuzi ya mtu mzima. Kwa makusudi yetu, uchangiaji una maana ya matumizi ya mafunzo ya nadharia ya mtu mzima kiutendaji ili kuwasaidia kujifunza. Mjadala uliopo chini unapitia matumizi ya mbinu hizi mpya za kujifunza kwa ajili ya jukumu la kuwalea wapanda Kanisa.

Shughuli:

1. Waombe washiriki kueleza kwa maneno yao wenyewe tofauti kati ya ufundishaji na uchangiaji.
2. Walize washiriki kuelezea tofauti kati ya kuwafundisha watu wazima na kuwasaidia watu wazima kujifunza. Ijapokuwa washiriki wengi wataelezea uchangiaji kama "kuwafundisha watu wazima," jibu halisi ni kwamba uchangiaji ni sanaa na sayansi ya *kuwasaidia watu wazima kujifunza*. Tofauti hii ni ya muhimu sana na sharti isisitizwe mara kwa mara.

### **DHANA ZA MSINGI KWA ELIMU YA WATU WAZIMA<sup>9</sup>**

Waelezee washiriki kwamba dhana ya uchangiaji iliasisiwa na mafunzo ya Malcolm Knowles na wenzake. Walisimamia mpango wao wa elimu ya watu wazima katika dhana nne zifuatazo, ambazo ni mapendekezo halisi yanayotumika kama msingi wa mwelekeo wao kwa elimu ya watu wazima. Tambulisha dhana hizi kwa washiriki.

1. Kadiri watu wanavyokomaa, wanapitia mabadiliko katika uwezo wao wa kufanya uchaguzi. Katika uchanga na utoto mtazamo uliopo ni ule wa utegemezi kabisa. Ukomavu huzalisha ufahamu wa kujitegemea na kujiongoza. Watu wazima wanafanya chaguzi na kukubali kuwajibika nazo. Ni katika hatua hii mtu husesabika kuwa mtu mzima kisaikolojia.
2. Kuingia katika utu uzima huongeza uzoefu mpya na wa aina mbalimbali. Maisha ya uzoefu ambayo mtu mzima huyaleta kwenye mchakato wa kujifunza huongeza ufanisi wa mwanafunzi kuhusiana na kufaidika na matukio mapya ya mafunzo. Benki hii au mkusanyiko wa uzoefu ni wa thamani sana kwa mtu mzima. Kwa bahati, mbinu za kimapokeo za kufundisha zinaongeza hali ya kujihusisha katika mbinu za kiujuzi zinazohamasisha matumizi, mwingiliano, na uchambuzi wa uzoefu wa mwanafunzi. Hii inamaanisha kwamba ujuzi wa kujifunza una mwelekeo wa aina mbili badala ya kuwa na miekeo mingi.
3. Kadiri mtu anavyokomaa, msukumo wa kufanya vitu kitaaluma hubadilishwa kwa shauku na motisha ya kujifunza kutegemeana na hitaji la ujuzi na uwezo mpya. Hii huhitajika ili mwanafunzi aweze kufanya vema katika majukumu yake mapya ndani ya jamii. Ni muhimu kwamba ujuzi mpya wa mafunzo uendane na maendeleo ya kazi inayohitajika.

---

<sup>9</sup> Imetolewa kutoka kwa Malcolm Knowles, *The Adult Learner: A Neglected Species*(1978:56-71)

4. Elimu ya asili au ya kimapokeo imejengwa juu ya somo. Mwalimu hueleza kozi ya mafunzo na masomo ambayo wanafunzi wanapaswa kujifunza ,kwa matumizi ya wakati ujao inavyowezekana. Watu wazima huingia katika fursa za kielimu kama mwitikio wa hitaji la uwezo mpya katika maeneo maalumu wanayohisi kupungukiwa. Kozi yao imejengwa juu ya matatizo au maisha. Kuna hali ya uharaka katika mafunzo ya watu wazima: kilichofundishwa leo kinatakiwa kitumiwe kesho na sio mbali kwa wakati ujao.

**Shughuli:** Fupisha dhana hizi kwa kifungu kimoja ili kusaidia kumbukumbu. Majibu ya washiriki yaendane na pointi hizi nne.

1. Watu wazima wana dhana binafsi ya kujiongoza wenyewe. (Mwongozo wa Mshiriki: "Watu wazima hufanya **CHAGUZI** na kukubali kuwajibika nazo.")
2. Watu wazima huuleta uzoefu na ujuzi wao kwenye mchakato wa mafunzo. (Mwongozo wa Mshiriki: "Watu wazima huulela **UZOEFU** wao kwenye mchakato wa mafunzo.")
3. Watu wazima huhamasika binafsi. ( Mwongozo wa Mshiriki: "Watu wazima **WANAHAMASIIKA** kujifunza ujuzi na uwezo unaohitajika.")
4. Kozi ya mafunzo ya mtu mzima inalenga matatizo au maisha. ( Mwongozo wa Mshiriki: "Elimu ya watu wazima imejengwa juu ya **MATATIZO** au **MAISHA**.")

Waombe washiriki walinganishe pointi hizi nne pamoa na orodha waliyoianadaa mwanzoni wa kipindi ya kuwasaidia watu wazima kujifunza na kuwafundisha watoto.Je, kuna pointi yoyote katika zilizopo juu imetajwa katika orodha hiyo?

#### **FAIDA YA KUWALEA WATU WAZIMA<sup>10</sup>**

Kanuni saba zilizojengwa juu ya dhana za kimsingi zimeorodheshwa chini. Kila kanuni itawasaidia washiriki kuelewa sifa za mlelewa na kuwezesha mchakato wa mafunzo.

#### **Kanuni ya kwanza: Watu wazima wanahitaji kujua **KWA NINI**.**

Ulimwengu unadalika mara nyingi, ukiwapa walelewa matukio mapya yanayohitaji mafunzo ya nyongeza. Kama watu wazima, watahitaji kujua kwa nini wajifunze kitu fulani kabla hawaajaingia katika hatua mpya ya mafunzo ambayo itaongezea mambo juu ya ratiba yao ambayo tayari imejaa mambo mengi.

**Faida |** Mlelewa huingia katika uhusiano wa malezi akiwa na ufahamu wa kwa nini jambo hili ni la muhimu.

---

<sup>10</sup> Imetolewa na kufupishwa kutoka kwa Knowles, Holton and Swanson (1990:57-63)

**Shughuli:** Waulize kwamba ni washiriki wangapi wanauliza swali la, "Kwa nini ninatakiwa kujifunza hili?" wanapofikia hatua mpya ya mafunzo. Je, kujibu swali hilo kunasaidiaje mchakato wa mafunzo? Je, kunasaidiaje uhusiano wa malezi?

Washiriki wanapoanza kushughulika na walelewa, walelewa wanapaswa kubaini sababu za kukua katika uwezo wao wa kupanda kanisa. Hamasa yao ni ipi?

### **Kanuni ya pili : Watu wazima HUJITAWALA na KUJIONGOZA.**

Watu wazima hupenda kujiongoza wenyewe. Walelewa wana dhana binafsi ya kuwajibika kwa kufanya maamuzi yao wenyewe na kuyaongoza maisha yao binafsi. Hii ina maana kwamba jaribio la kuwaingizia mawazo au dhana watu wazima lina kila dalili ya kukutana na upinzani. Watu wazima wanapenda kuheshimiwa na kuonekana kama wabia walio sawa katika tukio la kujifunza.

**Faida |** Walelewa wamechagua kozi hii ya vitendo kama chaguo bora la kuongeza ujuzi unaohitajika kwa wakati huu. Hii inajumuisha uhusiano wa mlezi na mlelewa wanaojihusisha na mwelekeo ule ule ,ambao katika hao mmoja ana ujuzi zaidi ili kuutumia kumwongoza mwengine.

**Shughuli:** Waulize washiriki uchaguzi huu chanya utakuwa na athari gani katika ujuzi wa malezi. Kwa mtazamo wa hili, ni kwa namna gani mlezi atahakikisha mlelewa anaongeza ujuzi unaohitajika kwa huduma pasipo kuharibu hali ya kujitegemea na mwelekeo wake binafsi. Je, kuna vidokezo hasi vinavyohusiana na tabia hii ya mafunzo kwa mtu mzima? Kama ndivyo, ishughulikiwaje? Ni muhimu kwamba walezi wawaulelewa kubainisha kile ambacho wangependa zaidi kujifunza, wangependa kukua katika ujuzi upi, na ni tabia zipi bainifu wangependa kuzishughulikia. Kuwapa walelewa orodha ya chaguzi mbalimbali kunaweza kufaa zaidi.

### **Kanuni ya tatu: Watu wazima wanamiliki hazina ya UZOEFU wa yaliyopita.**

Uzoefu wa awali wa mtu mzima anayejifunza unatoa raslimali za kutosha kujifunza. Watu wazima wanakuja katika shughuli za kujifunza wakiwa na ujazo mkubwa na uzoefu mbalimbali ulio bora tofauti na ule wa mtoto.

**Faida |** Uzoefu wa watu wazima wanaojifunza unatoa msingi wa maarifa wanayoweza kuyatumia katika matukio yanayotokea sasa. Uzoefu wa kutosha uliopatikana kwa kipindi kirefu cha maisha unamsaidia mwanafunzi kutathimini na kujilisha au kupata taarifa na ujuzi mpya. Kwa njia hii,ujuzi wa awali ni mawe ya kupandia kuelekea kwenye mageuzi ya mlelewa.

Shughuli: Mwombe mshiriki mmoja au wawili waeleze jinsi uzoefu usio wa kihuduma ulivyowasadida kutatua matatizo katika huduma au ulibadilisha mwelekeo wao kushughuka na watu katika huduma.

Inafaa walelewa kurejea uzoefu wa mambo yaliyopita (mambo waliyofanikiwa na waliyoshindwa), wajifunze kwayo, wamshukuru Mungu kwayo,na kumwomba Mungu awatumie kuwabariki wengine kwa wakati ujao.

**Kanuni ya nne: Watu wazima HULENGA TATIZO.**

Pale watu wazima wanapokutana na hali mpya ambayo hawapati jibu kuitia uzoefu wao uliopita, huweka mkazo katika kugundua njia mpya ya kushughulikia tatizo hilo. Kuufanya mchakato wa malezi ulenge kushughulikia matatizo yanayowahusu walelewa kutawafanya wauthamani zaidi.

**Faida** | Matatizo na hali zote katika huduma zinatoa mkazo wa uzoefu katika kujifunza. Walezi na walelewa wanatafuta suluhisho za vitendo kuliko kuitia nadharia zinazoweza ama zisizoweza kufaa kushughulikia tatizo lililipo.

**Shughuli:** Waombe washiriki kureja namna ambavyo uzoefu wao unaweza kuwa chombo cha kuwasaidia walelewa wao wapate suluhisho za vitendo kwa matatizo yaliyopo?

**Kanuni ya tano | Watu wazima wako TAYARI KUJIFUNZA.**

Watu wazima huwa tayari kujifunza hasa tu kwa mwitikio wa hali ambazo hawajajiandaa nazo. Hii hutoa msukumo unaohitajika ili kujifunza na kukuza ujuzi mpya unaowawezesha kukabiliana na hali hizo ipasavyo.

**Faida** | Walelewa huingia katika uhusiano wa malezi wakitafuta majibu ya matatizo ambayo tayari wameyabaini.

**Shughuli:** Elezea kwamba hii humaanisha kuwa kwa walelewa, uzoefu wa mafunzo unahusiana na hali halisi za maisha ambazo kwazo wanatafuta kukuza ujuzi mpya na uwezo unaohitajika katika huduma zao ama majukumu yao ya kijamii. Waulize washiriki kuwa ni kwa vipi hii inaifanya kazi ya malezi iwe rahisi zaidi.

**Kanuni ya sita | Elimu ya watu wazima HULENGA MAISHA.**

Kwa walelewa, elimu ni mchakato wa kukuza viwango vya uwezo ili kufikia uwezo wa juu zaidi. Hii ni kinyume kabisa na maelekezo ya mazingira yenye mkazo wa somo unaotokana na kujifunza kimapokeo.

**Faida** | Kama watu wazima, walelewa hulenga kazi au tatizo katika mazingira yao ya kujifunza. Wanatafuta majibu kwa hali halisi zilizopo Mara zote kuna hali ya uharaka- kile kilichofundishwa leo sharti kiwe na matumizi kwa hali iliyopo sasa.

**Shughuli:** Mruhusu mshiriki mmoja au wawili waeleze jinsi ambavyo kuitumia kanuni hii kunarekebisha dhana yao ya malezi.

**Kanuni ya saba: Watu wazima WANAHAMASIIKA BINAFSI.**

Hii ina maana kwamba hamasa ya walelewa ni ya ndani kuliko nje. Kujifunza kunathaminiwa kwa ndani kwa namna ya kujiheshimu, ubora wa maisha, kuridhika na kazi, na/au hali ya utimilifu

**Faida:** Walelewa wanaweza kuitikia baadhi ya aina ya hamasa za nje, lakini hamasa zenyenuguu zaidi ni misukumo ya ndani ili kukutana na malengo yao binafsi. Walezi hawatakiwi kufanya kazi kama wahamasishaji.

### **Muhtasari wa Kanuni saba**

Unapoendesa mafunzo,kumbuka maswali yafuatayo kuhusu kile ambacho kila kanuni inatufundisha juu ya walelewa: (1) Ni kwa jinsi gani taarifa hii inatoa miongozo kwa ajili ya mchakato wa malezi? (2) Ni kwa namna gani washiriki watahusianisha taarifa hii katika mwendo wao wa malezi?

Shughuli: Waulize washiriki namna ambavyo kile walichojifunza kwa habari ya uchangiaji ( kumsaidia mtu mzima kujifunza) kitabadilisha mwelekeo wao wa malezi. Kila mshiriki abinishe kitu fulani hasa kutoka katika kanuni hizi saba ambayo angependa kuiweka akilini anapotenda kazi pamoja walelewa.

Soma maswali haya sita ambayo mlezi anaweza kumuuliza mlelewa, na uwaulize ikiwa kuna maswali mengine ambayo washiriki wangependa kuyaongezea.

1. Kwa nini unajihuisha na mchakato wa malezi?
2. Je, ni ujuzi au taarifa zipi ungependa kujifunza?
3. Je, ni tabia zipi bainifu ungependa kuzikuza kwa miezi michache ijayo?
4. Je, ni tabia zipi bainifu ungependa kuzibadilisha kwa miezi michache ijayo?
5. Je, baadhi ya uzoefu wako wa awali wa maisha ni upi, na Mungu anawezaje kuutumia katika huduma yako?
6. Ni matatizo au changamoto zipi unakabiliana nazo kwa sasa katika huduma yako, uhusiano wako na Mungu, au familia yako?

### **CHANGAMOTO ZINAZOWAKABILI WATU WAZIMA**

Walelewa ni wanachama wa makundi tofauti ya watu wanaoshiriki wito mmoja. Wanatokea kwenye makundi mbalimbali ya kijamii, na makundi yenye uchumi na kazi tofauti. Viwango vyao vya elimu vinatofautiana, na hivyo uwezo wao kitaaluma na kiakili unatofautina. Kwa habari ya uzoefu, wanatofautiana kutoka kiwango cha viongozi wanaoingia na viongozi wa huduma waliokomaa. Baadhi watakuwa ndio wameanza safari yao ya kiroho hivi karibuni, wakati wengine watakuwa wamefurahia miongo kadhaa ya maisha ya Kikristo na huduma.

Kwa baadhi, huduma inawakilisha mabadiliko ya kazi katikati ya maisha. Wengine wameitwa katika umri mdogo kuingia katika huduma kama wapanda kanisa. Hakuna watu wawili watakuwa na talanta zote sawa, ujuzi, uwezo na karama zote sawa. Kitu hicho hicho ndicho chawea kunenwa kwa kundi ambalo Mungu ameliita kuwalea.

Mungu huwaita watu kutoka kila mwelekeo wa maisha na mazingira ya jamii.Baadhi ya walezi watakuwa na uzoefu wa kiuongozi na kihuduma kuliko wengine.Unaweza kuhitaji kukazia kwa washiriki kwamba si vyema kuwapa upendeleo zaidi walelewa wenye ujuzi zaidi

katika uongozi wa Kikristo au fursa zaidi za kielimu. Kwa hiyo, mkazo sahihi unapaswa uwe kuwajenga walelewa ili watimilize jukumu ambalo Bwana amewaitia, pasipo kujali walikotoka au hatua ya maisha waliyo nayo wanapoanza mchakato wa mafunzo.

**Shughuli:** Waulize washiriki watoe mfano wa mtu aliyekuja kwa Kristo akitokea katika mazingira yasiyopendeza, lakini kupitia ushawishi na pengine malezi ya Mchungaji na waumini wengine amekomaa kama kiongozi wa Kikristo.

### **CHANGAMOTO ZA KAWAIDA WANAZOKABILIANA NAZO WAPANDA KANISA**

Mchakato wa lazima wa mafunzo kwa ajili ya huduma na hatimaye kuingia katika wito huu kunampa mpanda kanisa mpya changamoto nyingine mpya. Mlelewa, inawezekana kwa wakati huu ni mtunza familia, mtumishi na mwanafunzi. Hii ni nyongeza ya majukumu na wajibu aliokuwa nao awali. Orodha ifuatayo inawapelekea washiriki kwenye mjadala juu ya magumu ambayo walelewa wanaweza kukabiliana nayo na kuyashinda. unapoipitia orodha, waalike washiriki waeleze kwa kifupi asili ya kila changamoto na kuongeza vitu vingine kwenye orodha ndani ya kila kundi.

**Shughuli:** Waombe washiriki wabaini changamoto ambayo walelewa wana mwelekeo wa kukabiliana nayo katika upandaji wa Kanisa.

#### **1. UWIANO wa majukumu yaliyopo**

- Familia
- Kazi
- Elimu, mafunzo ya kihuduma
- Kukua kiroho na afya
- Majukumu mengine ya kijamii
- Kusimamia muda

#### **2. Kusimamia FEDHA.**

- Nyumba
- Elimu
- Huduma
- Kazi (kwa wapanda kanisa wenye kazi nyingine)

#### **3. Kuongeza UJASIRI.**

- Changamoto za kielimu zinazohusiana na darasani na kazi nje ya darasa.
- Hofu ya kufeli
- Uwezo wa kihuduma

#### 4. Kuandaa **MFUMO** wa **MSAADAA**

- Marafiki na jamaa watakaota msaada wa kihisia kwa familia
- Wabia wa maombi na kikundi cha maombezi
- Mlezi.

#### 5. **KUWEKA MTANDAO** na wanafunzi wengine pamoja na wapanda kanisa.

- Wanafunzi wenzake
- Kundi la wapanda kanisa wenzake

Shughuli: Wagawe washiriki katika vikundi vitano na uwaagize kila kikundi kije na maoni ya kuwasaidia walelewa kushughulika na moja ya changamoto tano zilizoorodhesha juu.

#### **FAIDA NA THAWABU KUTOKA KWENYE MCHAKATO WA MALEZI**

Mpaka hapa, umeshawaongoza washiriki katika mjadala wa sifa za mtu mzima na kuzitumia taarifa hizi katika mchakato wa malezi. Orodha ifuatayo inakamilisha somo kwa kuitia baadhi ya faida wanazopata pande zote, kwa mlezi na mlelewa kutokana na uhusiano wa malezi.

Shughuli: Wagawe washiriki katika makundi mawili. Waombe kundi moja libainishe faida kwa mlelewa katika mchakato wa malezi. Waombe kundi jingine libainishe faida kwa mlezi. Linganisha orodha hizi na zilizopo chini (pia kwenye Mwongozo wa Mshiriki).

Mlelewa ata:

- Pata mtu wa kusaidia kushiriki mzigo
- Kuwa na uwezekano mkubwa zaidi wa kufanikiwa
- Kuwa na mtu wa kumwajibisha
- Ona ukuaji mkubwa na wa haraka wa kanisa jipya
- Pata manufaa ya kujifunza kutoka kwa mtu mwenye uzoefu zaidi
- Pata nafasi ya kuongeza mashauri yenyeh hekima
- Kuza uhusiano wa kiroho wenye maana utakaokuwa kielelezo cha huduma kwa siku za usoni
- Kuwa na mfano ufaao kwa ajili ya kuutumia kuwalea wengine kwa wakati ujao.

Mlezi ata:

- Pata furaha inayotokana na kupasisha uzoefu wake na maono yake
- Saidia kuwezesha ufalme wa Mungu kukua
- Tajirishwa kutokana na uhusiano wa malezi
- Ona ushawishi na ufanisi wa huduma yake ukizidishwa
- Epuka udumavu na inawezekana hata kuchoka mno
- Acha urithi udumuo

- Jifunza. Watu hujifunza vizuri zaidi kwa kufundisha
- Ongeza thamani yake kwenye ufalme wa Mungu.

### **HITIMISHO**

Mwisho wa kipindi , chagua shughuli moja au mbili kutoka mionganini wa zifuatazo ambazo zitawawezesha washiriki kulinganisha vema ujuzi wao wa mafunzo kwa vitendo kama walezi.

**Shughuli:** Waombe washiriki wabaini namna malezi yanavyochangia kukua kwa ufalme wa Mungu. Watie moyo wafikirie kwa mtazamo wa maendeleo ya uongozi na kukua kwa Kanisa.

**Shughuli:** Waombe washiriki wajadili moja ya maswali yafuatayo katika kikundi kidogo na kisha watoe taarifa kwenye kundi.


1. Pointi zipi katika kipindi hiki ni za muhimu zaidi kwako? Je, ni kwa vipi ufahamu wako kuhusu asili ya walelewa unakusaidia kuwawezesha wapanda kanisa wapya kujifunza?
2. Kama matokeo ya somo hili, je, mtazamo wako kwa habari ya malezi umebadilikaje? Utawaleaje wapanda kanisa kama matokeo ya kile ulichojifunza kuhusu tabia za walelewa?

### **MAOMBI YA KUFUNGA KWA WALELEWA NA WALEZI**

Mwombe mmoja wa washiriki aombe kwa ajili ya mahitaji ya walelewa ambao kundi litakuwa likiwalea. Mwombe mwingine awaombee walezi watakaokuwa wakiwekeza katika maisha ya wapanda Kanisa wanaolelewa.

## KIPINDI CHA TATU UHUSIANO WA MALEZI

Imesimamia katika Sura ya 2, 7, 9 na 10 ya *Masterful Mentoring*



### UTANGULIZI

Katika sura hii tutakuwa tukijadili aina ya uhusiano unaohitaji kuimarishwa ili malezi yaliyo bora yaonekane. Sio walezi na walelewa wote wanafahamiana vizuri. Hata kama wanafahamiana, wanaweza kuwa hawajamarisha uhusiano wa ndani na wenye uwazi ulio muhimu kwa malezi yaliyo bora.

Utakuwa ukiangalia maeneo matano hasa yanayohusiana na kuanzisha uhusiano wa malezi yenyen nguvi:

1. Sifa za mlezi mzuri
2. Sifa za mlelewa mzuri mzuri
3. Mahitaji ya mlelewa
4. Umuhimu wa kuaminiana na usiri
5. Agano la malezi

### SIFA ZA MLEZI MZURI

**Shughuli:** Anza kipindi kwa kuwauliza wale waliopo kwenye kikundi kufikiria siku zaz nyuma katika maisha yaohadi wakati amba mtu fulani aliwalea. Je, mtu huyu alikuwa mlezi mzuri? Kama ndivyo, ni mambo gani yaliyomfanya awe mlezi mzuri? Je, ni sifa gani za mlezi mzuri wanazozifikiria? Muwe na mjadala wa jumla juu ya swali hili kabla ya kuelekea katika uwasilishaji.

Walezi wazuri wanashiriki sifa fulani muhimu. Unapozipima baadhi ya sifa hizi, washiriki wazipitie na kuamua ikiwa, kwa tathimini yao binafsi, wanahisi kuwa wanazo sifa hizi muhimu.

#### 1. Mlezi mzuri ni **MSIKILIZAJI MZURI**

Kuna methali ya Kihispaniola inayosema namna hii: "Tuliumbwa na masikio mawili na mdomo mmoja tu. Kwa hiyo, basi, sharti tusikize mara mbili zaidi ya tunavyonena." Walezi wazuri wanasiliza zaidi kuliko wanavyoongea.

Wanapoongea, ni kwa kuuliza maswali ili wasikie majibu yanayotoka kwa walelewa.

Baadhi wameuita usikilizaji *madhubuti*. Wengine wanauita usikilizaji *makini*. Kwa kutumia vivumishi hivi, mkazo uko katika kitu kinachotenda kazi. Huu si usikilizaji tendewa, ambao wakati tunapoendelea na mazungumzo hatuzingatii kwa kweli miitikio kutoka kwa wenzetu. Katika usikilizaji tendewa, fikra zetu huhamia kwenye mambo mengine ama kwenye jambo tunalotaka kulisema baadaye. Lakini kwenye usikilizaji madhubuti au makini, tunaweka usikivu kwenye kile wanachosema wengine. Tunasoma

MWONGOZO WA MKUFUNZI | MALEZI

mawasiliano yasiyo ya sauti vilevile mawasiliano ya sauti, na kujaribu kuelewa kile wanachomaanisha na sio tu kuelewa wanachosema. Mtaalamu mmoja wa malezi aliita hii kama "kujihusisha na ulimwengu wa wanafunzi kiuhalisia na kujaribu kuupitia kutokea ndani."<sup>11</sup>

Shughuli:

- 1.Ukiwa na mwenye kujitolea kutoka kwenye kikundi, jenga usikivu hafifu na usikivu makini Anayejitolea akwambie juu ya nini alifanya mwisho wa wiki iliyopita wakati ukionyesha kwa vitendo usikivu hafifu (dhaifu) kwa kubadilisha somo, wala huzingatii kile anachokisema mhusika, na unazungumza yale uliyofanya wewe mwishoni mwa wiki iliyopita. Kisha toa kielelezo cha usikivu makini kwa anayejitolea akwambie yale atakayofanya leo na kesho, ukimuuliza maswali ili kubaini anachosema, ukimuuliza namna anvyopambanua hali mbalimbali ama kumuuliza anajisaje juu ya mambo mbalimbali. Tunza mwelekeo kwa kuelewa vyema kile anachojaribu kusema mhusika.
- 2.Waulize washiriki ikiwa wamewahi kufika katika hali ambayo, kwa kuisema tu hali yao kwa mtu mwengine, waliweza kuibua mpango wao wenyewe wa kutatua tatizo. Washiriki waeleze uzoefu wao kwa mtu mmoja au wawili waliokaa karibu nao. Ruhusu dakika kadhaa za kushirikishana.
3. Eleza kwamba, kwa nyongeza ya kutufanya kuelewa hali kutokana na mtazamo wa mlelewa, kuwa msikivu mzuri kunamsaidia pia mlelewa kuwa mtatuza wa matatizo kadiri anavyosema nia yake na kutathimini utatuza unaowezekana. Ikiwa walezi wanajihusisha zaidi na kuongea kuliko kusikiliza, walelewa wao hawawezi kufanya ugunduzi wao binafsi. Ugunduzi binafsi mara zote ni wa thamani zaidi kuliko kulishwa majibu kwa kijiko na mtu mwengine.

## 2. Mlezi mzuri hushughulika na mambo yanayotokea katika maisha kwa "**WAKATI**."

Katika mahusiano ya malezi,tunashughulika na nyakati za maisha za kupanda na kushuka, za matukio ambayo walelewa wanakabiliana nayo kwa wakati uliopo. Kwa mpangilio wa kielimu, "mafunzo ya wakati"-ambayo ni kushirikisha kitu kwa "wakati wa kufundishwa" ni ya ufanisi zaidi kuliko mafundisho yasiyokuwa na muunganiko ama uhusiano na hali halisi ya mlelewa ya wakati uliopo. Wakumbushe washiriki kwamba moja ya sifa ya mtu mzima ni kuwa na uwezo wa kuyatendea kazi mara moja yale anayojifunza. Ukweli huu ndio uliopo katika malezi. Malezi yanahitaji kurejea hali halisi ya wakati uliopo na siyo ya mbali, isipokuwa inashughulika na maono, ambayo kwa asili yanalenga wakati ujao. Hata

---

<sup>11</sup> Daloz, L. (1999). Effective teaching and mentoring. San Francisco: Jossey-Bass Publishers,p.205

<sup>12</sup>Havighurst, R. J.,(1972).Developmental tasks and education (3rd ed.). New York: McKay,page unkown

baada ya hapo, kuna hatua zilizopo zinazoweza kujadiliwa. Wataalamu wawili wa malezi wanaandika: "Walezi wazuri wanasaidia kuwiwekea nanga ahadi za wakati ujao"<sup>13</sup>

**Shughuli:** Waombe washiriki kadhaa waliowahi kuitia uzoefu wa mafunzo ya wakati washirikishe kikundi. Fuatilia kwa maswali zaidi,kama haya:

- Je, ni kwa namna gani mafunzo yako katika eneo hili yalikuwa ya tofauti na baadhi ya uzoefu wa mafunzo yako mengine?
- Je, unajisikia kwamba kama mtu mzima tunajifunza zaidi na kutunza mafunzo hayo pale yanapokuwa ya wakati?
- Je, unajionaje ukiyaweka kwenye matendo malezi yako mwenyewe kwa wakati unaokuja?

### **3. Walezi wazuri ni kama WAKUNGA**

**Shughuli:** Waulize washiriki majukumu ya mkunga ni yapi. Kisha waeleze kwamba walezi hutenda kazi kama wakunga, wakiwasaidia "watu wengine katika kuzaa mawazo mapya, ujuzi mpya, sura mpya, na njia mpya za kuwa na kutenda. Wanawasaidia wanafunzi katika kuzaa mawazo yao binafsi, maono na malengo."<sup>14</sup> Wape washiriki fursa ya kueleza kwa nini ni muhimu kwa walelewa kuongeza mawazo mapya, maono mapya, au malengo mapya.

### **4. Mlezi mzuri humsaidia mlelewa KUONA njia MBADALA.**

Eleza kwamba watu wanapokabiliana na hali ngumu, wanawaza KUBAKI wakiona utatuzi mmoja tu, matokeo ya aina moja tu, njia moja tu ya utendaji. Pale walelewa wanappojadili masuala fulani na walezi wao, mlezi anaweza kuwasaidia kuona njia mbadala. Wanaanza kuona kwamba kunaweza kuwa na utatuzi ambao hawakuufikiria, na wanaongozwa kufikiri kwa undani na kwa utofauti. Chemsha bongo inaweza kufanyika. Utaratibu wa ushirikiano wa watu wawili au zaidi kushughulika na hali fulani unaweza kuleta mawazo ya ubunifu na njia mpya za kufikiri ama kutenda mambo.

**Shughuli:** Toa mfano kutokana na uzoefu wako mwenyewe, kama inawezekana, ambayo kwayo uliongozwa kuona njia mbadala. Kisha waombe washiriki kutoa baadhi ya mifano yao binafsi juu ya jambo hili.

**Shughuli:** Waombe washiriki kubaini hali ambazo kwazo walelewa wanaweza kuhitaji msaada ili kuona njia mbadala.

Washiriki wapendekeze njia za kuwasaidia walelewa kufikiria njia tofauti za utatuzi, kama vile mlelewa kuorodhesha angalau njia tatu mbadala za kushughulikia tatizo. Walezi wanaweza kuwasaidia walelewa kugundua matokeo yanayowezekana kwa kila njia mbadala kwa kuuliza "Ukifanya hivi, nini kitatokea?"

---

<sup>13</sup> Parks,S.D & Parks, S. (2000). The big question,worthy dreams: mentoring young adults in thier search for meaning,purpose, and faith(1<sup>st</sup> ed.). San Francisco: Jossey-Bass Inc., p.128.

<sup>14</sup>Vogel, L. (2000). Reckoning with the spiritual lives of adult learners. New Directions for Adult and Continuing Education, 85 (Spirng), p. 24.

## **5. Mlezi mzuri ni MCHOCHEAJI.**

Sote tunahitaji mtu fulani anayetuamini. Tunamhitaji Barnaba anayeweza kututia moyo tunaposhushwa moyo na kujisia hali ya kushindwa katika huduma.

Shughuli: Nani aliye kuchocha katika safari yako ya kiroho? Kama ukimtaja mtu fulani, waambie washiriki habari za huyu mtu na jinsi alivyokuchocha. Kisha wagawe washiriki katika vikundi vidogo vya watu 3-4 and uruhusu muda wa wao kushirikishana juu ya "wachochearji" wao. Mwombe mshiriki mmoja au wawili walishirikishe kundi lote.

## **6. Mlezi mzuri ni mwenye KUFIKIRI kwa UMAKINI.**

Kama walezi, tunahitaji kuwasaidia walelewa kufikiri kwa umakini na kwa uchambuzi: mambo si marahisi na si dhahiri. Walezi wanapofikia utatuzi, watahitaji kuchambua hali iliyopo ili kuwasaidia walelewa wao kuvuka mipaka ya hali hii. Walezi wazuri wanawasaidia walelewa wao...

- Kubaini taarifa muhimu juu ya hali, ikiwa ni pamoja na chanzo chake. (Hii ni pamoja na nguvu ya upandaji wa Kanisa.)
- Kuiitikia hali hiyo ipasavyo
- Kubaini mtazamo wao
- Kufikiria mitazamo ya wengine
- Kufikiria mguso wa muktadha wa kiutamaduni juu ya watu wanaowahudumia.

Shughuli: Wape washiriki dakika 5 za kuitia kibinansi sifa hizi. Kisha waombe kugawanyika katika vikundi vya watu 2 au 3 watumie dakika 10-15 za kushirikishana juu ya sifa ipi waliyo nayo na sifa ipi wanayohitaji kuiboresha zaidi ili wawe walezi wazuri.

## **MAMBO YA KUEPUKA**

Kipengele hiki kingeweza kuitwa "Sifa za Mlezi Mbaya." Pitia orodha iliyo chini kwa kifupi ukiwa na washiriki pasipo kutumia muda mwingi mno, isipokuwa mtu katika kikundi anataka kwenda kwa undani zaidi. (Kumbuka: Kwa maelezo ya ukamilifu juu ya kila moja ya sifa hizi, angalia sura 7 katika kitabu Masterful Mentoring.)

- Kutoa ushauri kwa haraka na kwa urahisi mno.
- Kukosoa. Kukosoa huharibu uchunguzi
- Kuokoa. Tunajifunza zaidi kuto kana na makosa yetu kuliko tunapozuiwa kufanya makosa
- Kujenga mipaka isiyo ya lazima. Mara nyingi walezi tunaogopa kwamba walelewa wetu watatuzidi na kwa hiyo tunaweka vizuizi visivyo lazima ili kuzuia ukuaji wao zaidi
- Kupuuza swali la "kwa nini." Mara zote kuna sababu nyuma ya kila jambo.
- Kupunguza uzito wa jambo. Inadhalilisha tunapoacha kupo kea yale anayotuambia mlelewa. Kile kinachowezza kuwa mlima kwake sisi tunakiona si kitu, lakini kushindwa kushughulika na mlima kunamshusha mlelewa.

**MWONGOZO WA MKUFUNZI | MALEZI**

Tabia hizi sita zinaweza kupatikana kwa walezi "wenye sumu". Wanakatiza mafunzo ambayo yanetokea katika uhusiano wa malezi hata kabla hayajaanza.

Shughuli:

1. Washiriki waeleze tabia zilizopo juu kwa maneno yao.
2. Waulize washiriki wabaini ni sifa ipi kati ya sita wanapata shida sana kuionyesha, na kwa nini.Jadili jinsi ambavyo walezi wanaweza kuziepuka ama "kutoendeleza" tabia hizi.

### SIFA ZA MLELEWA MZURI

Mtu wa muhimu sana katika uhusiano wa malezi mazuri ni mlelewa. Mlezi mwenye hekima aliwahi kusema "Safari, hata hivyo, inamhusu msafiri na wala siyo msindikizaji"<sup>15</sup>

1. Mlelewa mzuri ni yule anayechukua **WAJIBU** kwa **MAFUNZO** yake mwenyewe.

Wakumbushe washiriki kwamba moja ya sifa za mtu mzima ni kujiongoza mwenyewe.Wanajua ni lini na wapi waende kwa ajili ya kupata msaada.Walelewa wazuri wanaamua kwa namna mbalimbali juu ya mahitaji ama matakwa yao binafsi. Walelewa, kwa pamoja na walezi wao wanaamua ni lini watakutana, watakutana mara ngapi, na watakapokutana kipindi kitachukua muda gani. Wanaweza pia kuamua mada ipi muhimu izungumziwe katika kipindi cha malezi, kutegemeana na matukio yaliyopo katika maisha yao.

2. Mlelewa mzuri **MSIKILIZAJI MAKINI**.

Walelewa,kama ilivyo kwa walezi wanapaswa kuwa "wasilikizaji makini". Walelewa wanahitaji kusikia yale ambayo walezi wao wanasema, na kisha waamue watafanya kwayo.

3. Mlelewa mzuri ni **MTENDAJI**.

Katika uchunguzi uliofanyika Chuo Kikuu cha Jimbo la Michigan, mlelewa/ mwanafunzi mtendaji alielezewa kama mtu ambaye...

- Hutafuta mrejesho wenye msaada na huonyesha kuutambua.
- Haogopi kuuliza chochote ambacho kwacho anahitaji kukua
- Haogopi kuuliza maswali.
- Hushiriki kikamilifu katika uhusiano wa malezi
- Huutumia sawasawa umahiri na uzoefu wa mlezi.

4. Mlelewa mzuri ni mwanafunzi wa **KUDUMU**.

Elezea kwamba wakati walezi wanapowasaidia walelewa wao ni mahali gani waende kwa ajili ya kupata msaada (masomo yaliyochapwa, Intaneti, watu wengine, nk.), wanawawezesha walelewa kuwa wanafunzi wa kudumu. Walelewa hawapaswi kuwa tegemezi kwa walezi, iwe kwa mwendo mfupi ama kwa kipindi cha muda mrefu.

---

<sup>15</sup> Daloz, L.(1999). *Effective teaching and mentoring*.San Francisco: Jossey-Bass Publishers,p.228.

Malezi huwasaidia walelewa kukuza nyenzo muhimu ili kuendelea kujifunza peke yao pasipo kuingiliwa na walezi wao.

#### 5. Mlelewa mzuri yuko **WAZI**.

Walelewa wazuri wako wazi na ni wakweli kwa walezi wao. Hawafichi taarifa muhimu. Walezi, kama madaktari, wanaweza kusaidia tu kutokana na taarifa zinazoshirikishwa kwa hiari, na wanaweza "kutoa tiba isiyo sahihi" ikiwa taarifa muhimu zitafichwa. Mlelewa mzuri atakuwa mkweli juu ya mapungufu na mahitaji na atayaeleza matatizo yake kwa uwazi.

#### SIFA ZA MLELEWA MBAYA

Sifa za mlelewa mbaya ni pamoja na zifuatazo:

1. Wanakuwa **TEGEMEZEI** mno kwa walezi wao ili kupata majibu.
2. Hawachukui hatua za **AWALI** kubaini maeneo mapya yanayohitaji kushughulikiwa kutokana na kudhihirika kuititia matukio katika maisha yao.
3. **WANAPUUZA** yale wanayosema walezi wao ama kushauri.
4. Wanashindwa **KUCHAMBUA** uhalisia wa hali ya wakati uliopo na kuona kule ambako wangepaswa kuwa.

Shughuli: Waulize washiriki ikiwa wanaweza kufikiria sifa nyingine za mlelewa mbaya. Waombe wapendekeze wanavyoweza ama wanavyopaswa kufanya wakati walelewa wanapoonyesha tabia hizi.

#### MAHITAJI YA WALELEWA

Katika kipindi hiki utakuwa ukijadili aina mbili za mahitaji ya walelewa: Mahitaji ya **KIMAHUSIANO** na mahitaji ya **KIMAFUNZO**

#### MAHITAJI YA KIMAHUSIANO

Walelewa wana maeneo makuu matatu ya mahitaji ya kimahusiano: kutembea kwao na Mungu, uhusiano wao na familia zao, na uhustiano wao na huduma yao ya upandaji wa kanisa.

Utaratibu wa kipaumbele cha mlelewa unapaswa kuwa **MUNGU** kwanza, pili **FAMILIA**, na **HUDUMA** iwe ya tatu. Je, ni kwa vipi matumizi yetu ya muda, fedha na raslimali zetu yanaonyesha vipaumbele vyetu? Jinsi tunavyotatua matatizo na kufanya maamuzi kunaakisi vipi vipaumbele vyetu?

**Shughuli:** Waombe washiriki kupendekeza maeneo ambayo mlelewa anaweza kuhitaji mwongozo. Wagawe washiriki katika vikundi vya 2-4 na uruhusu kama dakika 10 kwa vikundi kujadili haya na kuandika maoni haya.

Kisha waombe vikundi vyote kushirikisha majibu yao kwa kila mmoja. Andika maoni juu ya ubao au karatasi kubwa. Kisha kama kundi, amueni ikiwa kila moja ya majibu haya yanahusiana na maeneo ya Mungu, Familia, na/ama Huduma. Weka M mbele ya majibu yanayoshughulika na hitaji letu la uhustiano na Mungu, F kwa Familia na H kwa Huduma. Sisitiza umuhimu wa kumweka Mungu kwanza, kisha familia na mwisho huduma.

MWONGOZO WA MKUFUNZI | MALEZI

Shughuli:

1. Waulize washiriki kwa nini ni muhimu kwa walelewa kupanga utaratibu wa vipaumbele wakianza na Mungu kwanza, familia ya pili na huduma iwe mwisho.
2. Waombe walelewa kuchukua dakika chache kuchunguza maisha yao na kusikiliza kile ambacho Mungu anasema nao kwa habari ya vipaumbele vyao. Je, ni kweli wanamweka Mungu kwanza, familia ya pili na huduma ya tatu? Waite wafikirie juu ya ushahidi wa vipaumbele vyao. Ni kwa jinsi gani matumizi ya muda wao, fedha na raslimali vinaamua juu ya vipaumbele vyao? Jinsi wanavyotatua matatizo na kufanya maamuzi yao kunaakisi vipi vipaumbele vyao?
3. Waalike washiriki wawashirikishe wenzao kile walichokigundua juu ya vipaumbele vyao na wabaini kile wanachohitaji kufanya ili kudumu katika vipaumbele vyao ama badiliko wanalo hitaji kulifanya ili kurekebisha vipaumbele vyao.

## MAHITAJI YA KIMAFUNZO

Mahitaji ya kimafunzo ya walelewa yako matatu: maarifa, ufahamu na ujuzi. Kwa maneno mengine, walelewa kama wanafunzi wanahitaji maarifa fulani ya masingi. Wanahitaji kufahamu thamani ya mafunzo hayo, na wayatumie pale wanapoweza. Mwisho, wanapaswa kukuza ujuzi wao wa huduma. Walezi waaweza kuwasaidia walelewa wao katika maeneo haya yote matatu.

Shughuli: Waombe washiriki waorodheshe angalau mifano 2 kwa kila mahitaji haya ya kimafunzo ya walelewa. Yaandike haya juu ya ubao ama karatasi kubwa. Katika eneo la maarifa, mahitaji ya kimafunzo yatapimwa kwa mafunzo wanayopitia kwa njia ya masomo ya vitendo. Kwa habari ya ufahamu, wanathaminije, kwa mfano, hitaji la kuwa na maono yaliyo wazi au kuandika kauli ya dhima? Juu ya ujuzi, je wanaweza kufafanua maono yao kwa wengine kwa namna inayolewaka na kwa ufupi? Je, wanaweza "kuyauza maono" katika kikundi cha watu?

## KUAMINIANA NA USIRI

Uhusiano wa malezi umejengwa juu ya kuaminiana na utunzaji wa siri. Ikiwa moja ya maadili haya mawili itakosekana, uhusiano utadhoofika, na kushindwa vibaya kutatokea.

Shughuli: Waulize washiriki maneno *kuaminiana na usiri* yanamaanisha nini kwao. Kisha waulize kwa nini haya ni ya muhimu sana ili kuwa na uhusiano wa malezi wenye afya.

Katika kipindi hiki, kwanza tunajadili mambo ya kufanya na yasiyopaswa kufanya katika maeneo ya kimahusiano na kiujuzi yatakayosaidia kujenga kuaminiana na siri katika uhusiano wa malezi. Hatimaye, tunajadili usiri.

## MAMBO YA KUFANYA NA YASIYOPASWA KUFANYA KATIKA MAHUSIANO.

### 1. HESHIMU: Usidunishe

Walezi wanahitaji kuwaheshimu walelewa wao, wakiwaruhusu kuwa wakweli na wawazi pasipo hofu ya kudhalilishwa. Wawe makini na hisia za walelewa wao, usoefu, na jitihada na waimarishe yaliyo mema, na kusahihisha kwa upole na kwa heshima.

## **2. THAMINI: Usishushe thamani**

Kila mmoja anapenda kuthaminiwa kama mtu. Walezi hawapaswi kuwa mabwana kwa walelewa wao, wala wasinyooshe vidole vyao kwa walelewa kwa habari ya yanayowezekana kuyaboresha. Zaidi, wanahitaji kuwathamini walelewa wao kama watu.

**Shughuli:** Washiriki waangalie katika Wagalatia 5:13; Waefeso 5:21; Warumi 12:10 na kujadili namna ambavyo mistari hii inavyohusiana na pointi hii.

## **3. UWE KIELELEZO: Usiingilie**

Yesu alikuwa kielelezo cha huduma na tabia kwa wanafunzi wake. Walezi wanapaswa kufanya vivyo hivyo. Wanapaswa pia waepuke kuingilia mambo ya walelewa katika maeneo ambayo hawakuruhusiwa.

## **4. IMARISHA: Usihukumu**

Shughuli: Washiriki wasome kwa sauti vifungu vifuatavyo: Warumi 14:13; Warumi 15:7; Waefeso 4:32. Waombe kuelezea jinsi ambavyo vifungu hivi vinahusiana na kuimarisha na sio kuhukumu.

## **5. TIA MOYO: Usikatishe tamaa.**

Wakumbushe washiriki kuwa walezi mara nyingine wanaweza kuwa msaada ama kikwazo kwa walelewa wao.

Shughuli: Soma 1Wathesalonike 5:11pamoja na washiriki. Waombe washiriki kufikiri juu ya maandiko mengine yanayoweza kutumika.

## **6.CHOCHEA: Usipunguze.**

Walezi wanapaswa kuwaambia walelewa wao, "Unaweza kufanya!" mara nyingi zaidi ya kuwaambia, "Mmm, inaonekana shughuli haiwekani kwako."

**Shughuli:** Waulize washiriki ikiwa wamewahi kukutana na mtu mkatisha tamaa, mtu ambaye mara zote huwashusha watu chini ama aliyewaambia kuwa wangeshindwa kwa kila walilofanya. Je, walijisikiae? Je, "ushauri" huu uliawatia moyo kujaribu, au uliwakatisha tamaa? Nini hutokea ikiwa mtu anaendelea kukatishwa tamaa?

## **7. OMBA: Usidhalilishe**

Paulo ananena na Wakristo wa Filipi, "Kuwahesabu wengine kuwa bora kuliko nafsi yako" (Wafilipi 2:3). Kudhalilisha maana yake ni kushusha au kumtendea mtu mwengine kwa hali ya dharau au dhalili. Ni hali ya kujihesabu sisi kuwa bora kuliko wengine.

Shughuli: Waulize washiriki namna ambavyo maombi yanaweza kuwaepusha walezi kuwa wadhalilishaji kwa walelewa wao.

## **MAMBO YA KUFANYA NA YASIWAPASWA KUFANYA KUHUSIANA NA UJUZI.**

### **1. SIKILIZA: Usizungumze**

Kumbuka, watu wana masikio mawili na mdomo mmoja tu. Je, hiyo inatuambia nini kwa habari ya uhusiano wa malezi?

Shughuli: Waulize washiriki kuwa elimu yao binafsi ilihuksikaje walipokuwa na mwalimu ambaye alizungumza yeye tu. Je, walitiwa moyo kujifikiria wenyewe, ama ni kufuatisha yale tu ambayo mwalimu alikuwa ameyasema? Je, huku ni kujifunza kweli, au ni "kusema" tu pasipo matokeo ya kudumu?

## **2. ULIZA: Usieleze**

Je, walezi watapambanuaje yale wanayohitaji walelewa wao ikiwa walelewa wanasikiliza tu mazungumzo ya walezi. Walezi wanapaswa kuuliza maswali zaidi kuliko kutoa majibu. Ugunduzi binafsi hutokea pale walezi wanapouliza maswali kwa walelewa wao badala ya kuwaambia nini cha kufikiri ama cha kufanya.

## **3. ELEZA WAZI: Usidai**

Walezi sharti wawe na uhakika wanaelewa yale wanayohitaji walelewa wao na yale wanayotafuta. Vinginevyo, walezi wanawenza kutoa majibu yaliyoandalila kwa hali isiyo sahihi, wakitoa hekima wasiyoihitaji walelewa.

## **4. CHOTA: Usimimine**

Walezi wanapaswa kuchota kutoka kwa walelewa taarifa inayohitajika ili kusaidia. Hawapaswi kumimina tu taarifa kwa walelewa wao.

**Shughuli:** Waulize washiriki kwa nini watu huona ni rahisi tu kumimina taarifa ndani ya kichwa cha mtu mwengine. Je, walezi wanafikiri kwamba kwa kutumia njia ya mkato, walelewa watajifunza mambo mengi zaidi na kwa haraka zaidi?

Shughuli: Uliza ikiwa kuna washiriki walishawahidi kwenda na swali kwa mtaalamu wa kompyuta. Labda walitaka kujifunza tu namna mfumo fulani unavyofanya kazi, kama vile kutuma hati kwenye printa. Badala yake, mtaalamu akaimiliki kompyuta mwenyewe na kwa haraka akagonga vitufe na hati ikaanza kuchapwa. Na mshiriki akaachwa hali amekaa pale na mdomo ukiwa wazi hajui tena hata namna ya kuchapa hati kuliko hata kabla ya kuomba msaada kwa mtaalamu. Je, ni kwa namna gani mwanafunzi kama huyu atakuwa amejifunza cha zaidi? Je, badala yake huyu mtaalamu wa kompyuta atakuwa amefanya kitu gani? Je, mfano huu unawezaje kutumiwa katika dhana ya "kuchota"?

## **5. Uwe na AJENDA: Usiende kwenye kipindi cha malezi pasipo mpango kazi.**

Ajenda zinawasaadida watu kubaki njia kuu. Ajenda inaweza kuhusisha mambo yafuatayo:

- Mlelewa aombe, akisihii uwepo na uongozi wa Mungu kwenye mkutano. Ombeni wakati wowote kozi inapoendelea katika mkutano. Kamwe hatuwezi kuwa na maombi mengi kupita kawaida!
- Uliza mambo yanayomhangasha mlelewa -hata kama hii itasababisha kutokukamilisha ajenda za mambo mengine
- Fuatilia mambo mliyofanya kipindi kilichopita. Pitia na kuimarisha mafunzo yaliyopita. Angalia maendeleo ya mlelewa juu ya hatua za vitendo kutoka kwenye kipindi kilichopita.

- Wasilisha mawazo mapya uliyopenda kuyashirikisha
- Mlelewa abainishe pointi za vitendo za kushughulikia kama matokeo ya kipindi hiki.
- Omba kwa ajili ya mlelewa, kwa ajili ya mambo yaliyojiteza wakati wa kipindi, na kwa ajili ya pointi za vitendo ambazo mlelewa atazishughulikia.

Ajenda inaweza kusaidia mambo kuendelea mbele vizuri wakati wa kipindi cha malezi. Walakini, mlezi hapaswi kuwa mtumwa wa ajenda, hasa ikiwa mlelewa akija na hitaji la lazima na la haraka.

#### **6. Toa MUDA: Usitumie mikato**

Walezi wawe tayari kuwekeza muda inavyotakiwa ili kukuza uhusiano wa malezi. Wasijaribu kutumia njia za mkato. Inachukua muda kujenga hali ya kuaminiana na usiri-haitokei kwa usiku mmoja.

#### **7. ONGOZA: Usiswage**

Walezi ni waongozaji; hawawaswagi walelewa na fimbo. "Wanawasaidia watu wengine kuzaa mawazo mapya, ujuzi mpya, mifano mipyga, na njia mpya za kuwa na kutenda"<sup>16</sup>

#### **8. RUDIA: Usiache kukazia.**

Kila mara walezi na walelewa wanapokutana pamoja, wanapaswa kuititia mafunzo yaliyopita na ukuaji. Kukazia ni kifaa cha kufundisha kiwango kinachoweza kuwasaidia walelewa kukumbuka dhana mpya, kuyaweka mafunzo mapya katika matendo, na kukuza hali ya kuwa kielelezo.

#### **9. Uwe RASLIMALI: Usitafiti**

Walezi wanapaswa kutumika kama raslimali, vilevile kuwaelekeza walelewa kwenye raslimali zingine. Walezi hawapaswi kufanya utafiti wao wenyewe: walelewa wao ni watu wazima na wana uwezo wa kujiongoza wenyewe.

Shughuli: Waombe washiriki waorodheshe raslimali kwa ajili ya walelewa. Raslimali hizo ni pamoja na watu wengine, vitabu, majarida, mikanda ya picha, mikanda ya sauti, tovuti, na blogu.

#### **10. Toa MTAZAMO: Usitoe majibu ya papo kwa papo.**

Walezi wawasaidie walelewa wao kuona uwezekano wa mambo, kufungua milango mipyga, na kuwatazamisha kwenye fursa mpya. Ijapokuwa, hii haimaanishi kwamba wanapaswa kutoa majibu kwa urahisi.

---

<sup>16</sup>Vogel, L. (2000). Reckoning with the spiritual lives of adult learners. *New Directions for Adult and Continuing Education*, 85 (Spring), p. 24.

Shughuli: Washiriki wajigawe katika vikundi vya watu 2-4 ili kujadili ni mambo yapi ya kimahusiano na kiujuzi ya kufanya na ya kuepuka kati ya yaliyotajwa hapo juu yenyeye ushawishi zaidi katika kujenga hali ya kuaminiana. Kwa maoni yao, ni mambo gani ya kuepuka ambayo yangesababisha hali ya kujenga kuaminiana kuwa ngumu zaidi, kama si kutokuwezekana? Ni mambo gani ya kufanya yaliyo muhimu sana katika mchakato wa kujenga hali ya kuaminiana?


### USIRI

Pasipo kuaminiana, haiwezekani kuwepo hali ya kutunziana siri. Pasipo usiri, imani yote hypotea. Vyote vinaenda mkono kwa mkono. Hakuna uhusiano wa kimalezi utakaokuwa bora ama utakaodumu ikiwa kilichosemwa sirini hakibaki sirini, au mlelewa anahisi kwamba usiri hautakuwepo. Hata pale walezi wanapodumisha usiri, ikiwa walelewa wao wanaamini usiri haupo, walelewa wataacha kushirikisha mambo yao kwa uwazi. Na hapo uhusiano wa kimalezi kamwe hautafikia masuala ya moyoni ama kufikia hali ya uwazi.

Kwa bahati mbaya, baadhi ya walezi wanakosa ukomavu wa kiroho na kihisia ulio wa lazima kwa ajili ya usiri. Hawajakomaa vya kutosha kuwapa ushauri walelewa wao katika njia zilizo nzuri na zenye kujenga. Mara nyingine wanazivumisha taarifa walizozipokea kutoka kwa walelewa wao, ama wanazitumia kinyume na walelewa wao, na hivyo wanawazuia walelewa wao kupiga hatua.

Shughuli: Waombe washiriki washirikishe mifano ya hali- pasipo kutaja ama kuelezea mambo kwa undani-ambayo kwayo kuaminiana kulipotea kwa sababu ya kukosa usiri. Je, ilikuwa ni kwa sababu ya masengenyo? Je, mlezi alivumisha hali aliyyoshirikishwa? Ama taarifa iliyoshirikishwa kwa siri katika uhusiano wa malezi iliwekwa hadharani au kunaswa tena kichwani kwa mlelewa? Je, kulikuwa na athari gani kwa mlelewa kwa kukosa usiri- na kwa mlezi- katika masuala haya?

### MKATABA WA MALEZI



Majadiliano katika kipindi hiki yanalenga hitaji la waleza na walelewa kuanzisha mkataba au agano kati yao. Ukweli, uhusiano wa malezi una maeneo matatu: Mungu, mlezi, na mlelewa. Waeleezee washiriki kwamba wanaingia kwenye agano la kiroho na walelewa wao: agano lenye maeneo matatu kati yao, walelewa na Mungu.

---

[Zingatia: Mchoraji atatengeza pembetatu yenyeye pande 3 zilizo sawa, yenyeye MUNGU kwa upande wa juu, FAMILIA upande wa chini kulia, na HUDUMA upande wa chini kushoto. Kwenye Mwongozo wa Mshiriki, itaonekana pembetatu tu, hivyo washiriki watapaswa kuandika maneno wao wenyewe]

## MAMBO YALIYOMO NDANI YA MKATABA WA MALEZI

Waelezee washiriki kwamba mikataba ya malezi inaweza sheria za msingi kwa ajili ya uhusiano wa malezi. Mkataba unajibu maswali yafuatayo:

1. Je, tutakutana lini na wapi?
2. Je,tutakutana kwa muda gani?
3. Je,tutakutana kila baada ya muda gani?
4. Tutakuwa na mada zipi katika vipindi vyetu?
5. Ni mada zipi,kama zipo,zitakuwa mwiko?
6. Je,kuna sheria zipi za kutunza siri?
7. Je,tutajuaje kwamba tumekamilisha kile tulichopanga kukifanya?

Pale mlezi na mlelewa wanapokamilisha malengo ya uhusiano wao wa malezi, wanaweza kuamua ikiwa wanataka kuendelea kukutana pamoja. Kama ndivyo, basi wanaweza kuandaa mkataba mpya wa malezi. (Kwa walelewa waliosajiliwa katika Mafunzo ya mpanda kanisa ya Mtando wa Kuzidisha, upandaji wa Kanisa mwishoni mwa kozi ya kumi na mbili unaashiria mwisho wa mchakato wa malezi).

Wasaidie washiriki walelewe kwamba haiwezekani mara zote kuzama katika majadiliano ya malezi kama walezi watakavyoona ni lazima. Kunaweza kuwa na baadhi ya mambo ambayo mlelewa hatapenda kuyashirikisha, hasa ikiwa mlezi pia ndiye Mchungaji wa mlelewa. Hii inaweza kuwa ni kwa sababu mlelewa anaona kwamba Mchungaji/ mlezi anaweza kutumia pointi hizi kwenda kinyume naye (mlelewa) kwa wakati ujao.

Elezea kwamba HAKUNA MALEZI yanayoweza kuwepo mpaka maswali yote saba yaliyopo juu yamejibiwa. Majibu ya maswali hay ndipo yanapotumika kama msingi wa uhusiano wa malezi. Kushindwa kufikia yale mliyoamua hufanyika kuwa msingi kwa ajili ya tathimini mpya ya uhusiano wa malezi. Ni jambo la hekima kwa walezi na walelewa kuupitia mkataba wao mara kwa mara. Kwa walelewa walio katika mpango wa Mtando wa Kuzidisha, hii itakuwa mwishoni mwa kila mtaala wa tatu wa mafunzo.

**Shughuli:** Waombe washiriki kusoma tena mambo 7 yaliyomo ndani ya mkataba wa malezi. Waalike kuchangia mambo mengine ambayo walezi na walelewa wanapaswa kukubaliana kabla ya kukutana.

## MUHTASARI WA KIPINDI NA KUHITIMISHA KWA MAOMBI.

Shughuli: Katika kufunga kipindi hiki cha uhusiano wa malezi, waombe watu wajitolee kubaini pointi za msingi zilizofundishwa. Kisha tumieni muda pamoja katika maombi kwa ajili ya walezi, walelewa, na kukua kwa hali ya kuaminiana na usiri katika mahusiano ya washiriki wa malezi.

## KIPINDI CHA NNE

### MAMBO YA MSINGI KUHUSIANA NA MALEZI

Imesimamia katika *Masterful Mentoring*, Sura ya 2 na Kiambatisho



### UTANGULIZI

Katika kipindi hiki utawasaidia washiriki kuelewa misingi ya kipindi cha malezi yenyewe. Utapitia maudhui ya malezi-maeneo ya maisha ya kiroho, maisha ya familia na maisha ya huduma-vilevile kuangalia maswali yatakayotumiwa kutathimini maeneo yote kati ya haya matatu. Umuhimu wa kuanzisha pointi za vitendo zitakazofikiwa katikati ya vipindi umekaziwa. Kwa nyongeza, kipindi hiki kitajadili uthamani wa kitabu cha malezi, vilevile faida ya wataalam wengine katika mchakato wa malezi.

### MAUDHUI YA KIPINDI CHA MALEZI

Kipindi cha malezi kinashughulika na maeneo matatu hasa:

- Maisha ya kiroho ya mlelewa
- Maisha ya kifamilia ya mlelewa
- Maisha ya kihuduma ya mlelewa

### MAISHA YA KIROHO

Walezi wanahitaji kuwasaidia kuelewa kwamba uhusiano wao endelevu na Mungu ni kitu cha msingi sana kwa mafanikio yake katika huduma. Mahitaji yanayohusiana na kiroho kwa walelewa yanapaswa kuwa kipaumbele: viongozi wengi wa kiroho wameshindwa katika nyumba zao na katika huduma kwa sababu ya udhaifu wa kiroho. Migandamizo ya upandaji kanisa katika mazingira fulani inataka kutembea kwa ukaribu na Mungu. Kwa sababu hii, walezi wanahitaji kuwa wasikivu hasa kwa kile ambacho Mungu anakisema na kukifanya katika maisha ya walelewa.

Walezi wanapaswa kuwauliza walelewa wao aina ifuatayo ya maswali:

- Mungu anasema nini na wewe kwa wakati huu? Je, unatambuaje hili?
- Je, Mungu amekufundisha nini tangu kipindi chetu cha mwisho?
- Je, ungetathiminije kutembea kwako na Mungu kwa wakati huu: ni kwa ukaribu, ni hafifu, ama ni kwa mbali?

Kingine kilicho muhimu sawa ni kuumbwa kwa tabia ama makuzi ya tabia ya mlelewa. Kipindi cha malezi kinawenza kushughulika na maswali yanayohusiana na nidhamu za kiroho, kama vile:

- Je, una muda wa kutulia pamoja na Mungu kila siku? Nielezee.
- Je, unaunganishaje nidhamu yako ya maombi na kufunga katika maisha yako unapopanda kanisa hili?
- Je, unatenga muda kutoka katika shughuli za kihuduma na kuwa na faragha peke yako, ukitafuta sauti ya Mungu? Elezea hili.
- Nieleze juu ya maeneo yoyote unayopambana kiroho?

- Unafanya nini kujilinda mwenyewe kutoka katika vishawishi vinavyoweza kutunasa kirahisi na kuharibu ushuhuda wetu mbele ya wengine?

Hii ni mifano tu ya aina ya maswali yanayoweza kuulizwa kwa habari ya maisha ya kiroho ya mlelewa.

Shughuli: Shirikiisha mifano ya maswali ambayo washiriki wanaweza kuwaaliza walelewa kwa habari ya maisha yao ya kiroho. Kazia kwamba maswali maalumu kuhusiana na mwenendo wa kiroho wa mlelewa yanaweza kupatikana kwenye Sanduku la Nyenzo.

([www.multiplicationnetwork.org](http://www.multiplicationnetwork.org))

**Zingatia** | Ikiwa walelewa wataungama dhambi katika maisha yao, itahitaji busara ya walezi kuona namna ya kulishughulikia hili, kwanza kwa upande wa usiri na katika kuwashauri walelewa kwa kusudi la kuwarejesha upya. Walezi wanapaswa kuwatia moyo walelewa wao kuungama dhambi kwa Mungu, kuiacha, na kutoa fidia au malipizi ikiwezekana kama ishara ya toba yao.

#### MAISHA YA KIFAMILIA

Walezi wanahitaji kuuliza maswali kwa habari ya mahusiano ya walelewa na wenzi wao na watoto wao. Lakini walezi wanapaswa kufanya kwa tahadhari na kwa uangalifu sana wanaposhughulika na masuala haya ya ndani. Kusudi la malezi ni kuwasaidia walelewa na sio kuwaumiza. Maswali ya walezi hayapaswi kuonekana ya kidadisi; bali, yawape walelewa fursa ya kushirikisha furaha za maisha ya kifamilia na magumu ambayo inawezekana yanajitokeza, lakini katika mazingira ya kuaminiana na usiri kwa kiwango ambacho kwacho walelewa watajisikia kufarijika.

Shughuli: Waulize washiriki ikiwa wanajisikia amani kuuliza maswali yanayohusu maisha ya kifamilia ya walelewa wao. Wadhani ni maswali gani yanayofaa, na ni maswali gani wanajisikia ni ya miiko? Je, ni mipaka gani ambayo walezi hawapaswi kuivuka?

Shughuli: Wagawe washiriki katika vikundi vya watu 2-3 na uwaombe watengeneze mfululizo wa maswali kwa habari ya maisha ya kifamilia. Wape kama dakika 15 kwa shughuli hii. Kisha andika maswali watakayoyaibua juu ya ubao ama karatasi kubwa.

Vikundi vinaposhirikisha majibu yao, chunguza ili kuona kama maswali yafuatayo yametajwa. Kama sivyo, hakikisha unayataja wewe mwenyewe.

- Je, unatoa muda gani kwa familia yako, ukilinganisha na huduma? Je, ungelisema ni asililia ngapi ya muda unaitoa kwa kila moja?
- Je,wewe na mwenzi wako mna muda maalum kila juma ambapo mnajitenga peke yenu ili kujenga uhusiano mpya? Tafadhalii nishirikishe kuhusu yale mnayofanya.
- Watoto wenu wanajisikiaje mnapokuwa na muda kwa ajili yao?
- Je,huwa unafanya mambo gani kuifanya nyumba yako iwe mahali salama kwa ajili ya familia yako? Je,unailindaje nyumba yako isiwe nyumba ya hadhara, yenyе kutembelewa daima na wale unaowahudumia?

- Je, unashughulikia masuala yoyote ya kifamilia yanayozua uwezo wako wa kuwa fanisi katika upandaji wa kanisa?

Maswali ya nyongeza yanaweza kupatikana kwenye Sanduku la Nyenzo.

#### MAISHA YA KIHUDUMA

Ijapokuwa lengo kuu la mafunzo haya ni kuhakikisha makanisa yenyе afya yamepandwa, maswali ya awali yanalenga kudumisha afya ya *wapanda kanisa*. Maisha yao ya kiroho na kifamilia yanachongwa sawasawa katika mchakato wa kupanda kanisa. Ndio maana kipindi hiki kinashughulika na maeneo hayo mawili kwanza. Maswali kwa habari ya huduma ya upandaji kanisa yenyewe ni hatua ya tatu; ujuzi unaohitajika kupanda kanisa na hali halisi iliyopo ya huduma ya upandaji wa kanisa ni masuala yanayoweza kushughulikiwa kwa urahisi. Nia na shauku ya wapanda kanisa itakuwa mbali na huduma zao ikiwa hawakuyajali maisha yao ya kiroho na ya kifamilia kwanza.

Shughuli: Waombe washiriki wapendekeze baadhi ya videokezo vya huduma ambavyo walezi wanahitaji kuvikamilisha katika kipindi cha malezi. Viandike kwenye ubao au karatasi kubwa.

Elezea kwamba walezi wanaweza kuuliza maswali yanayoshughulika na maendeleo ya kanisa lililopandwa, muktadha ambao ndani yake kanisa jipya limepandwa, vizuizi ambavyo vimeibuka tangu kipindi cha kwanza cha malezi, na furaha ambazo walelewa wao wamekuwa nazo tangu kipindi cha mwisho. Kusudi la mapitio haya ya maisha ya kihuduma ni ili walezi wawe na mtazamo mpana wa hali iliyopo ya kanisa lililopandwa na wa mambo ambayo walelewa wao wanafanya ili kupanda kanisa jipya.

Baadhi ya maswali yanayoweza kutumiwa kuwasaidia walelewa kuchunguza maisha yao ya kihuduma:

- Je,unaweza kuniambia juu ya ziara ya ushuhudiaji uliyoifanya hivi karibuni? Iliendaje, na kwa nini?
- Je,kuna mapambano ambayo umekuwa ukikutana nayo kwa sasa katika upandaji wa kanisa? Tafadhali nielezee juu ya hili.
- Je,umefanya ziara ngapi tangu tulipokutana mara ya mwisho, na ni ziara ngapi umezifanya kwa kusudi la ufuatiliaji?
- Unafanya nini ili kulifahamu eneo vizuri?
- Ni kitu gani kipya umejifunza kuhusu eneo lako lengwa?
- Umekuwa na mafanikio kiasi gani katika kuanzisha kikundi kidogo?
- Je,kuna migogoro yoyote iliyojiteza? Kama ndivyo, uliishughulikiae?
- Je, unaona watu kwenye kikundi chako ambao ni viongozi wenye uwezo? Nielezee juu yao.
- Je,unajisikia faraja kiasi gani kwa namna ambayo kanisa linapandwa?
- Je,kuna eneo lolote la kihuduma ambalo unajigundua binafsi kutokuwa na amani nalo, ama ungehitaji msaada?
- Ni nani umewaomba wawe wasaidizi wako wa maombi unapopanda kanisa hili? Je,ni mara nyingi kiasi gani unawajulisha mahitaji ya kuombea na majibu yake?

**Zingatia** | Walezi wanapaswa kuwa wasikivu kwa mahitaji yasiyotarajiwa pale walelewa wanapokuja katika kipindi cha malezi. Inawezekana kuna kitu kinawabana-kinawasumbua au hata kinawapa furaha- ambacho walelewa wangependa kukishirikisha mara moja. Hii inapotokea, walezi wanapaswa kuweka kando agenda zao kwa kitambo na kushughulikia hali hii. Vinginevyo, hawataweza kufanikiwa sana katika kipindi hiki, kwa kuwa walelewa hawataweza kuwa na umakini huku wakitamani kuwaeleza walezi wao kile kinachoendelea, kiwe kizuri ama kibaya. Huu unaweza kuwa muda wa kujifunza ambao walezi hawapaswi kutokutilia maanani.

Pia, ni muhimu kuuliza maswali yanayohusiana na ripoti ambazo walelewa wanapaswa kuziwasilisha mwanzoni mwa kila kipindi. Walezi wanaweza kupanga kuzipitia wakiwa pamoja na walelewa wao ili wawe kama ubao wenye kumbukumbu kwao.Uaminifu wa walelewa kurejesha ripoti hizi itakuwa kama pimajoto ya kuumbika kwa tabia zao na kiwango cha nidhamu katika kufanya kile kinachopaswa kufanya.

Shughuli: Ogne na Nebel katika kitabu chao kiiwacho, *Empowering Leaders Through Coaching*, wanajadili mambo sita ambayo walezi waelekezaji wanaweza kuyafanya wakiwa pamoja na walelewa wao: sikiliza,sherehekea, jali, panga, funza na tia changamoto. Je, kila moja ya matendo haya yanahusika na nini.

## POINTI ZA VITENDO

Kipindi cha malezi hakijakamilika pasipo mlezi kuuliza swal, 'Kwa hiyo,hatua zako zinazofuata ni zipi?' Walelewa watiwe changamoto kufikiri na kuamua yale watakayofanya baadaye,ikiwa yatahusiana na maisha yao ya kiroho,ya kifamilia au ya kihuduma.

Kupanda kanisa ni mwendelezo wa shughuli. Walelewa wanahitaji kufikiri ni nini watakachofanya baadaye ili kushughulikia masuala ya maisha yao na Mungu, kuimarisha maisha yao ya kifamilia na kuendeleza kanisa linalopandwa.

Masuala mbalimbali yanapoibuka wakati wa kipindi,yanapaswa kushughulikiwa kwa njia fulani; walelewa wanahitaji kuamua ni kwa vipi na lini. Kujifunza halisi hutokea pale tu walelewa wanapowajibika na kukua kwao. Hii hukamilishwa kwa hatua maalum za vitendo. Hatua hizi vilevile hutumika kama vipimo imara ambavyo walezi na walelewa kwa pamoja wanaweza kupima maendeleo yaliyofikiwa.

Maswali yafuatayo yanaweza kuwasaidia walelewa kuweka orodha ya hatua za vitendo:

- Ni hatua zipi utakazochukua kuhusiana na hali hii?
- Ni kitu gani unataka kukamilisha kati ya sasa na kipindi kijacho tutakapokutana?
- Je,unaona ni kitu gani kinachofuata ambacho unahitaji kukifanya kuhusiana na hali hii?
- Unatumaini kusuluhishaje mgogoro kati ya [jina] na [jina]?
- Unatumaini kuvuka vipi katika kizuizi hiki?
- Ni mambo gani matatu unajikia kuyafanya ili kuliendeleza kanisa kati ya sasa na kipindi kijacho tutakapokutana?
- Utafanya kitu gani juma lijalo mkiwa pamoja na [jina] ili kufungua njia za mawasiliano?

- Je utakwenda wapi( au kwa nani) ili kupata msaada kwa tatizo ulilolitaja?

Kujibu maswali haya kutahitaji baadhi ya marejeo na kisha baadhi ya vitendo kwa upande wa mlelewa. Hawawezi kuwa wanafunzi wa kukaa au kutendewa tu.

**Shughuli:** Waombe washiriki waongeze maswali ya nyongeza kwenye orodha. Wakumbushe kwamba watapata maswali mengine ya msaada kwenye Sanduku la Vifaa. Waulize ni hatua ngapi za vitendo zitakuwa ni idadi nzuri kwa kila kipindi, na ikiwa walelewa watapaswa kubaini hatua za vitendo kwa kila eneo ( Mungu, familia,huduma).

#### **KITABU CHA TAARIFA CHA MLEZI**

Walezi wanapaswa kujua ni nini kinacholeweka katika vipindi nya malezi. Lakini, ikiwa kinafanikiwa kwa mpanda kanisa zaidi ya mmoja, walezi wanaweza kuchanganyikiwa kwa urahisi juu ya kile kinachotokea kwa mlelewa mmoja na mwininge ikiwa hawana nafasi ya kupitia vipindi. Tunapendekeza matumizi ya kitabu cha kumbukumbu cha mlezi

Katika kitabu cha mlezi, mlezi ananukuu ni lini alipokutana na mlelewa, kile kilichojadiliwa,na hatua zipi za vitendo zilizokubaliwa. Kitabu hakipaswi kiwe kitu chenye utata; inahitajika pawe ni mahali unapotunza rekodi ya mambo ya msingi. Hii itakusaidia kufuatilia mambo ambayo hayakushughulikiwa na kuwa na uhakika wa kusimamia hatua za vitendo mlizokubaliana. Vilevile kitabu kinaweza kutumiwa kama kumbukumbu ya maombi. Usiandike kwenye kitabu wakati wa kipindi, bali fanya hivyo mara tu baada ya mkutano.

Kabla ya kipindi cha malezi kinachofuata, walezi sharti wapitie yale yaliyotokea kwenye kipindi kilichotangulia. Pia wanapaswa kurejea maswali kwenye ukurasa wa pili wa kitabu cha mlezi, yanayoweza kutumika kama maoni ambayo kwayo wataawuliza walelewa kwenye kipindi kijacho.

Shughuli: Endesha igizo fupi ambalo kwalo utaonyesha mfano wa kukutana na mlelelewa. Washiriki wafanye mazoezi ya namna ya kujaza kitabu cha mlezi kuhusiana na mkutano huo. Kisha washirikishane wao kwa wao yale waliyoandika kwenye kitabu.

#### **KUWATUMIA WATAALAMU**

Kutoka wakati mmoja hadi mwininge katika kipindi cha malezi, walezi wanaweza kujisikia kuzidiwa ufahamu. Walelewa wao wanaweza kuhitaji nasaha au ushauri katika maeneo ambayo mlezi anajisikia kupungukiwa. Inapotokea, walezi wanahitaji kuwa wa kweli juu ya hili. Sisi sio wazoefu wa maeneo yote ya kihuduma.Walezi wazuri wanajua wakati wanapohitaji kuwapendekeza watu wengine wanaoweza kuwasaidia walelewa wao katika eneo fulani-watu walio wataalamu katika eneo la uhitaji. Hii pia inaweza kuwa malisho au msaada kwa wakati ujao. Mlezi anaweza kuuliza maswali kama, "Kwa hiyo, mazungumzo yako na Frank yaliendaje kuhusiana na tatizo uliloliletu wakati uliopita? Je, kuna chochote ungependa kukishirikisha?"

**Zingatia** | Walezi wanahitaji kutambua mipaka yao hasa katika eneo la ushauri. Ni watu wachache wenye mafunzo ya kutosha kufanya zaidi ya kutoa ushauri wa kawaida tu. Walezi ni muhimu wajue wakati wa kumpeleka mlelewa kwa mtaalam wa ushauri<sup>17</sup>. Kushindwa kufanya hivyo kunaweza kusababisha madhara kwa mlelewa na hata kumpelekea mlezi kuwajibika kisheria katika mazingira fulani.

Kwa kuzingatia upande chanya, hata hivyo, kumleta mtaalamu katika maeneo ambayo walezi hawajisikii amani nayo au hawajisikii utoshelevu kwayo, kunawaruhusu walelewa kupanua mitandao yao. Mmoja kati ya watu ambao mlezi hupendekeza anaweza kuwa mlezi wa walelewa anayefuata pale uhusiano wa sasa wa malezi utakapoisha.

## KUFUNGA

**Shughuli:** Waombe washiriki waandike kitu watakachofanya kama matokeo ya kipindi hiki ambacho hawakuwa wamekifirkiria hapo kabla. Waalike wachache ili washirikishe mawazo yao kwenye kundi lote.

---

<sup>17</sup> Kwa mfano, msaada wa mtaalamu utahitajika inapoonekana kuna masuala ya kibinagsi au ya kifamilia yaliyokosa ufumbuzi ambayo yanahitaji ushauri mpana zaidi. Wakati yanapokuwepo masuala nyeti ya ndoa au masuala yanayoonekana kwa kujirudia, mlezi wa kawaida anaweza asiwe na ujuzi wa kutosha wala asiwe na muda wa kushauri.

## KITABU CHA TAARIFA CHA MLEZI

Jina la Mlelewa \_\_\_\_\_

Tarehe ya Kukutana \_\_\_\_ / \_\_\_\_ / \_\_\_\_ Muda wa Kukutana \_\_\_\_ : \_\_\_\_ Mahali \_\_\_\_\_

**SWALI LA AWALI:** Je, ulijifunza nini katika kipindi chako cha mwisho? Je, umewezaje kukifanya kazi ulichojifunza?

MASWALI YA KIROHO (Maswali ya mfano yapo upande wa nyuma wa karatasi hii)

---

---

---

---

---

MASWALI YA KIFAMILIA(Maswali ya mfano yapo upande wa nyuma wa karatasi hii)

---

---

---

---

---

MASWALI YA KIHUDUMA(Maswali ya mfano yapo upande wa nyuma wa karatasi hii)

---

---

---

---

---

**KILA WAKATI:** Je, umerejesha taarifa yako ya ABC kwa kiongozi wako wa huduma?

HATUA ZA VITENDO (unapaswa kujaza kujaza pointi hizi pamoja na mlelewa wako)

---

## MASWALI YA KIROHO

- . Je, Mungu anasema nini na wewe kwa wakati huu?
- . Mungu amekufundisha nini tangu kipindi kilichopita?
- . Je, waweza kutathiminije kutembea kwako na Mungu kwa muda huu? Ni kwa ukaribu, ni hafifu? Ni kwa mbali?
- . Je, una muda wa kutulia pamoja na Mungu kila siku? Nieleze.
- . Je, ni kwa jinsi gani maombi na kufunga vina umuhimu kwako unapopanda kanisa hili?
- . Je, unatenga muda kutoka katika shughuli za kihuduma na kuwa na faragha peke yako, ukitafuta sauti ya Mungu? Elezea hili.
- . Shirikisha eneo lolote ambalo unapambana nalo kiroho na ambalo ungependa kunishirikisha.

## MASWALI YA KIFAMILIA

- . Je, unatoa muda gani kwa familia yako, ukilinganisha na huduma? Ni asilimia ngapi ya muda wako unaweza kusema unawapa?
- . Je,wewe na mwenzsi wako mna muda maalum kila juma ambapo mnajitenga peke yenu ili kupata chakula pamoja au kahawa na "kuhusiana upya" baada ya juma lenye mambo mengi? Je,waweza kuelezea yale mnayofanya?
- . Je, unaweza kusema watoto wako wanautathiminije muda unaoutoa kwa ajili yao?
- . Je,huwa unafanya mambo gani kuifanya nyumba yako iwe mahali salama kwa ajili ya familia yako? Je,unailindaje nyumba yako isiwe nyumba ya jamii, yenye kutembelewa daima na wale unaowahudumia?
- . Je, unashughulikia masuala yoyote ya kifamilia ambayo unahisi yanazuia uwezo wako wa kuwa fanisi katika upandaji wa kanisa? Shirikisha kile unachohisi unaweza.

## MASWALI YA KIHUDUMA

- . Niambie juu ya ziara ya ushuhudiaji ulioifanya hivi karibuni?
- . Shirikisha mapambano uliyo nayo nayo kwa sasa katika upandaji wa kanisa hili.
- . Je,umefanya ziara ngapi tangu tulipokutana mara ya mwisho? Ni ziara ngapi kati ya hizi zimekuwa ni fursa za ufuatiliaji?
- . Je, unafanya nini ili kulifahamu eneo vizuri?
- . Ni kitu gani kipyta umejifunza kuhusu eneo lako lengwa?
- . Je, unaona watu kwenye kikundi chako amba ni viongozi wenyewe uwezo? Nieleze habari za mmoja wao.
- . Je,unajisikia faraja kiasi gani kwa namna kanisa linavyopandwa?
- . Je,kuna eneo lolote la kihuduma ambalo unajigundua binafsi kuwa dhaifu ama kutokuwa na raha nalo?
- . Ni nani umewaomba wawe wasaidizi wako wa maombi unapopanda kanisa hili?
- . Hatua za vitendo
- . Unatumaini kuvuka vipi katika kizuizi hiki?
- . Je utakwenda wapi ili kupata msaada kwa tatizo ulilolitaja?  
Ni kitu gani unataka kukamilisha kati ya sasa na kipindi kijacho tutakapokutana?
- . Je,unaona ni hatua ipi inayofuata kuhusiana na...?

## ABC ZA MPANDA KANISA

### TAARIFA YA KILA MWEZI

#### TAARIFA YA JUMLA

MWEZI WA RIPOTI	
JINA LA MPANDA KANISA	
KANDA ANAYOTOKEA	
MRATIBU WA KANDA	

#### TAARIFA ZA BINAFSI

WATU WAPYA ULIOWAFIKIA WATU ULIOWAFIKIA KATIKA MAZINGIRA YA UPANDAJI KANISA	
WATU WALIOMPOKEA YESU WAFUASI WA YESU	
WATU WAPYA WALIOBATIZWA WATU WANAOSHIRIKI KATIKA SAKRAMENTI YA UBATIZO	
VIONGOZI WAPYA WANAOENDELEA NA MAFUNZO WATU AMBAO MPANDA KANISA ANAWAFUNZA KWA AJILI YA UONGOZI	

**VIKUNDI VIDOGO |** Angalau wanafunzi wapya 2 na kiongozi 1

VIKUNDI VIDOGO VIPYA VIKUNDI VILIVYOANZISHWA MWEZI HUU	
WASHIRIKI WAPYA KATIKA VIKUNDI VIDOGO WATU WAPYA WANAOSHIRIKI KATIKA VIKUNDI VIDOGO MWEZI HUU	
VIONGOZI WAPYA KATIKA KIKUNDI VIONGOZI WAPYA KATIKA KIKUNDI CHINI YA UONGOZI WA MPANDA KANISA	

#### MAHITAJI YA KUOMBEA

1. \_\_\_\_\_
2. \_\_\_\_\_
3. \_\_\_\_\_

#### SHUHUDA

---

---

---

---

---